Public Disclosure Authorized
Public Disclosure Authorized
Public Disclosure Authorized
Public Disclosure Authorized

82678

# Toleo Lililorahisisishwa Uchunguzi wa Matumizi ya Pesa za Umma

**Tathmini ya Bajeti:**
*Matumizi Yenye Matokeo Bora*

2013

TOLEO MAARUFU



JAMHURI YA KENYA
WIZARA YA UGATUZI NA MIPANGO

**Kuchapishwa na Serikali ya Kenya Septemba, 2013**

© Jamhuri ya Kenya

Wizara ya Ugatuzi na Mipango

JAMHURI YA KENYA

# TOLEO LILILORAHISISHWA UCHUNGUZI WA MATUMIZI YA PESA ZA UMMA

***Tathmini ya Bajeti:***
*Matumizi Yenye Matokeo Bora*

## TOLEO MAARUFU

*Octoba 2013*

# YALIYOMO


**DIBAJI** i

**MUHTASARI** ii

**UTANGULIZI** v

Sura ya 1. Muongo wa Maendeleo: Faida Mara Tatu 1

Sura ya 2. Mambo Muhimu ya Sekta 5

Sura ya 3. Makadirio ya Wakati wa Wastani: Mfumo wa Fedha Wasukwasukwa 31

Sura ya 4. Matumizi yenye matokea bora 39

Sura ya 5. Tamati 51


**VIELELEZO**


Kielelezo 1: Kupunguza pengo kati ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo 2

Kielelezo 2: Miundo misingi na maendeleo ya rasilimali inachukua zaidi ya asilimia 50 ya jumla ya bajeti ya sekta 3

Kielelezo 3: Wafadhili wanakidhi takriban asilimia 33 ya matumizi ya maendeleo, hasa miundo misingi 4

Kielelezo 4: Kupungua kwa fedha za wafadhili kama sehemu ya jumla ya bajeti 4

Kielelezo 5: Barabara na nishati zinachangia asilimia 80 ya jumla ya matumizi ya miundo misingi 6

Kielelezo 6: Uwekelezaji katika barabara hasa umelenga maendeleo 6

Kielelezo 7: Uwekezaji katika sekta ndogo ya kawi umelenga hasa usambazaji wa umeme kote nchini 7

Kielelezo 8: Kulinganishwa kwa viashiria vya miundo misingi nchini 7

Kielelezo 9: Asilimia 18 ya Wakenya wanapata maji ya bomba ikilinganishwa na asilimia 56 ya nchi za kipato cha kati 9

Kielelezo 10: Upatikanaji wa maji katika kaunti 9

Kielelezo 11: Karibu robo tatu ya bajeti ya maji huenda katika huduma za usambazaji wa maji 10

Kielelezo 12: Gawo la matumizi ya serikali naya wafadhili katika sekta ya maji 11

Kielelezo 13: Kenya inaendelea vyemaikilinganishwa na nchi zingine tukiangazia wauguzi na vitanda kwa kila watu 10,000 12

Kielelezo 14: Wanaochangia mzigo wa magonjwa 13

Kielelezo 15: Watoto waliochanjwa kikamilifu kwa kaunti (Miezi 12-23) 13

Kielelezo 16: Matumizi ya serikali katika sekta ya afya kama asilimia ya jumla ya bajeti 14

Kielelezo 17: Japo sehemu kubwa ya fedha za wafadhili kuelekezwa nje ya mifumo ya serikali, nyumba nchini bado zina mzigo mkubwa wa huduma za afya 15

Kielelezo 18: Asilimia 40 ya matumizi ya sekta ya afya inatumiwa kwa mishahara 15

Kielelezo 19: Wastani wa mgawo wa matumizi ya afya kwa ajili ya tiba na kinga haijabadilika 16

Kielelezo 20: Mgawo wa sekta ya kilimo, Shilingi bilioini (Bajeti ya maendeleo na ya kwaida) 17

Kielelezo 21: Matumizi ya sekta ya hifadhi ya jamiikama asilimia ya jumla ya bajeti ya serikali 2009/10 - 2010/11 17
Kielelezo 22: Walengwa wa OP-CTP kwa kaunti kufikia Juni, 2012 18
Kielelezo 23: Utekelezaji wa bajeti umeboreka….lakini kuna tofauti ya asilimia 20 katikati ya bajeti ya kwaida na ya maendeleo 19
Kielelezo 24: Tofauti zilizofichika za utekelezaji wa bajeti za sekta, 2005-2010 20
Kielelezo 25: Utekelezaji wa sekta ya miundo misingi 20
Kielelezo 26: Kiwango cha ufyonzaji wa fedha zilizotengwa katika bajeti katika sekta yaafya 21
Kielelezo 27: Ulinganishi wa mapato na matumizi 21
Kielelezo 28: Kwa wastani asilimia 47 pekee ya mikopo ya nje na misaada hutolewa, hii hudhoofisha utekelezaji wa bajeti ya maendeleo 22
Kielelezo 29: Udhaifu katika mifumo ya usimamizi ya fedha za umma 22
Kielelezo 30: Maendeleo ya deni la taifa la Kenya 24
Kielelezo 31: Mtungo wa madeni ya ndani umebadilika 24
Kielelezo 32: Utendaji wa mapato na matumizi ya Kenya ikilinganishwa na nchi zingine 25
Kielelezo 33: Upungufu katika mapato yameendelea tangu 2008/09 26
Kielelezo 34: Mchango kwa jumla ya mapato ya kodi 26
Kielelezo 35: Ongezeko katika matumizi ya umma yalileta kuimarika kwa ukuaji wa Pato la Taifa katika mwaka wa 2009-2011 27
Kielelezo 36: Njia ya ugavi wa mapato unatenga asilimia 23 ya mapato ya serikali kwa ajili ya serikali za kaunti 31
Kielelezo 37: Mapato ya kodi ya nyongeza ya thamani yataongezeka iwapo bidhaa zote zitatozwa kodi 32
Kielelezo 38: Madai ya mshahara wa wafanyikazi wa Kenya yakilinganishwa na nchi nyingine za Afrika (Kama asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali) 33
Kielelezo 39: Madai ya misharaha yaongezeka 34
Kielelezo 40: Serikali za kaunti zitapata Shilingi bilioni 210 ambazo magavana wanalalamika kuwa hazitoshi 34
Kielelezo 41: Mgawo wa kila mtu kwa kaunti 2013/14 37
Kielelezo 42: Sekta ya elimu yaongoza katika utekelezaji wa bajeti, 2005-2010 39
Kielelezo 43: Kuongeza mgawo kwa ajili ya elimu ya bure ya sekondari 41
Kielelezo 44: Ulinganishi wa matumizi ya sekta elimu na viwango vya elimu, 2010 41
Kielelezo 45: Asilimia ya wanafunzi wanaoweza kufuzu katika mtihani wa hesabu wa darasa la pili 43
Kielelezo 46: Mahali walipopatikana walimu wakati wa uchunguzi 44
Kielelezo 47: Uwezekano wa kukosekana shuleni 46
Kielelezo 48: Matokeo ya walimu wa shule za umma katika kujua silabasi na ujuzi wa kufunza 46
Kielelezo 49: Tofauti kubwa katika uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi katika viwango vya kaunti 48

## JEDWALI


Jedwali 1: Takwimu za mahitaji na matumizi 8
Jedwali 2: Matumizi kwa ajili ya sekta ya maji ikilinganishwa na Jumla ya Pato la Taifa na Jumla ya matumizi ya umma 10
Jedwali 3: Mwelekeo wa viashiria muhimu vya afya 12
Jedwali 4: Hesabu ya malipo ya wafanyikazi kwa kiwango cha juu zaidi katika jumla ya bajeti ya sekta ya elimu 40
Jedwali 5: Indiketa muhimu za elimu kwa mataifa kadhaa (2009) 42
Jedwali 6: Ulinganishi wa pembejeo za elimu kwa viwango vya kitaifa 43
Jedwali 7: Viwango vya kukosekana shule kulingana na aina ya shule 45
Jedwali 8: Ulinganishi wa pembejeo za shule kulingana na kaunti 48


## VISANDUKU


Sanduku 1: Ajenda ya mfumo wa ununuzi wa umma, Kenya 23
Sanduku 2: Malengo kadhaa ya kifedha ya muda wa wastani 35


## VIAMBATANISHO


Kiambatanisho 1: Bajeti ya 2009/10 – 2012/13 54
Kiambatanisho 2: Makadirio ya bajeti ya sekta mbalimbali, Shilingi bilioni 55
Kiambatanisho 3: Tofauti kati ya mapato hasa na viwango vilivyolengwa 56
Kiambatanisho 4: Ongezeko la thamani ndogo za ushuru zikilinganishwa na misingi yake 57
Kiambatanisho 5: Pendekezo la Kodi ya Nyongeza ya Thamani 2012 58
Kiambatanisho 6: Fomyula ya kukadiria kielezo cha kodi kinavyokabiliana na kupanda kwa pato la taifa 58
Kiambatanisho 7: Sera za kifedha zimetumika kuchangamsha ukuaji wa uchumi na kuudumisha 60
Kiambatanisho 8: Pengo kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo linapungua 60
Kiambatanisho 9: Sekta ya miundo misingi narasilimali za kibinadamu zinachukua zaidi ya asilimia 50 ya jumla ya bajeti 61
Kiambatanisho 10: Budget execution … recurrent and development 61
Kiambatanisho 11: Tofauti zilizoko katika utendekazi wa bajeti, 2005 - 2010 61
Kiambatanisho 12: Pengo la mapato ambalo limedumu tangu mwaka wa 2008/09, Shilingi milioni 62
Kiambatanisho 13: Kupungua kwa misaada ya wafadhili 62
Kiambatanisho 14: Kiambatanisho 14: Ulinganishi wa matumizi ya elimu na viwango vya kusoma na kuandika 63

# DIBAJI

Toleo hili maarufu ni muhtasari wa Ripoti ya Tathmini ya bajeti ya mwaka 2013 (Comprehensive Review ya Matumizi ya Umma—CPER) iliyotengenezwa na serikali katika kipindi cha miaka mitatu.

Ripoti hii inatoa ujumbe muhimu zilizomo katika ripoti kuu katika lugha rahisi ilikuwasaidia wananchi kuelewa matokeo ya CPER 2013. Aidha, inaonyesha mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali na matokeo ya utafiti wa kufuatilia matumizi ya umma/utafiti wa viashiria vya utoajiwa huduma (Service delivery indicator survey) (public expenditure tracking survey) katika sekta ya elimu.

Ripoti imetolewa wakati ambapo nchi inaingia katika Mpango wa pili wa Kipindi cha Kati (Medium Term Plan—MTP) ya Dira ya Kenya mwaka 2030. Wakati huohuo, ripoti imetolewa wakati nchi inafanya mabadiliko makubwaka tika mfumo wa usimamizi wa fedha kukiwemo mchakato wa kukabidhi mabadiliko yaliyotungwa na Katiba ya Kenya ya mwaka 2010. Uchambuzi unatoa uzoefu katika matumizi na mafanikio ya kwanza ya Mpango wa Muda wa Kati (MTP) itakayo kuwa msingi wa usimamizi wa fedha katika mpango wa pili wa MTP.

Matumizi ya serikali katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita imeshuhudia ongezeko kubwa katika matumizi ya maendeleo na ya kawaida. Hivyo basi, ripoti hii inatizama matumizi ya sekta na sehemu za serikali ya matumizi ya fedha zilizotengwa na wakati huohuo kuunganisha matumizi na mafanikio ikizingatia gharama yakufikia matokeo.

Maandalizi ya tahmini ya bajeti (PER) daima ni mchakato wa mashauriano ambayo yanahusisha wadau wote katika serikali, washirika wa maendeleo (Benki ya Duniana na GIZ) na wananchi. Katika miaka mitatu ijayo, serikali italenga utafiti shirikishi na uchambuzi katika sekta mbalimbali kama njia ya kuandaa hati/ ripoti ijayo. Serikali ina tambua kuwa msaada mkubwa kutoka kwa washirika wa maendeleo haupo kwenye bajeti, kila mwaka. Sisi kwahivyo tutafanya kazi na wadau wote ili kuteka matumizi yote kwa gharama za umma na kuhakikisha mafanikio na ufanisi wa fedha zote zilizotengwa.

**ANNE WAIGURU, OGW**
*Katibu katika baraza la mawaziri*
Wizara ya Ugatuzi na Mipango

# MUHTASARI

**Kenya imeweza kupata faida mara tatu kutokana na uerevu katika usimamizi wa sera za hazina ya serikali.** Miaka kadhaa iliyopita imeweza kushuhudia kuboreshwakwa matumizi ya bajeti ya maendeleo, utekelezaji bora wa bajeti na kupungua kwa kiwango cha deni la kitaifa kama sehemu ya Pato la Taifa. Vilevile, nchi imeweza kukusanya kiwango kikubwa cha ushuru kilicho juu kulingana na viwango vya nchi za Afrika zilizo kusini mwa jangwa la Sahara.Hata hivyo, mafanikio haya ya kusifika yanaweza kudhuriwa na: hatari kutokana na kuzidi kupungua kwa uzalishaji wa mapato, kupanda kwa madai ya mishahara, na hali ya wasiwasi katika mienendo na uwezo wa matumizi ya bajeti kwa serikali mpya za majimbo.

**Hapo awali, msimamo wa sera uliokuwa na viwango duni vya akiba na uwekezaji ulisababisha ukuaji wa uchumi kwa kiwango kidogo (miaka ya 1990s na 2000s).** Hata hivyo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, bajeti imefanyiwa mabadiliko makubwa yaliyopendelea uwekezaji, na hasa katika miundo misingi. Kwa mfano, matumizi ya maendeleo yameongezeka kutoka chini ya asilimia 4 ya Pato la Taifa (2005) hadi asilimia 10 ya Pato la Taifa (2012). Hakika, hatua hii kubwa ilitoa kichocheo kilichohitajika sana kwa uchumi wa Kenya na hasa katika miaka migumu ya 2008-2011 iliyokumbwa na majanga ya ndani (mgogoro uliokuwa baada ya uchaguzi na ukame) na nje (kupungua kwa uchumi wa biasharanje). Kipengele kingine cha bayana cha upanuaji huu wa miundo misingini ongezeko kwa Pato la Taifa la Kenya.

**Kenya sasa inauwezo wa kuongeza matumizi ya bajeti ya maendeleo** kwa sababu imeweza kutengeneza nafasi ya fedha za serikali kwa kupunguza deni la taifa na kuzuia kupanda kwa matumizi ya kawaida. La mno, jumla ya deni la taifa lilipunguzwa kutoka asilimia 63 ya Pato la Taifa(mwakawa 2000) mpaka asilimia 44 ya Pato la Taifa(mwaka wa 2012). Kupungua hukukwa deni hili kungeweza kuwa juu zaidi kama uchumi haungepatikana na majanga katika miaka ya 2008-2011. Katika kipindi hicho, matumizi ya kawaida yalipungua kutoka asilimia 24 ya Pato la Taifa katika miaka ya 1990 hadi asilimia 20 ya Pato la Taifa kufikia mwaka wa 2002.

**Kwa bahati nzuri, ongezeko la matumizi ya maendeleo kunasaidiwa nakuboreshwa kwa utekelezaji wa bajeti.** Kenya, kwa miaka mingi, imekuwa ikikumbana na utekelezaji duni wa bajeti uliosababishwa na maswala mengi, pamoja na matatizo ya kutekeleza mfumo wa ununuzi, mipango dhaifu, na uwezo mdogo wa utekelezaji na kadhalika. Hata hivyo, juhudi zakubadili hali hii iliokuwa kwa muda mrefu zimeanza kulete mafanikio. Viwango vya utekelezaji wabajeti, kwa mfano,vimeboreka: kutokaasilimia ndogo ya 55 mwaka wa 2005 hadi asilimia ya juu ya 70 mwaka wa 2011 kwa matumizi ya maendeleo. Katika kipindi hicho, matumizi ya kawaida yalikuwa na

wastani wa asilimia 95. Hata hivyo, katika mkusanyiko huu mpana, kuna tofauti za ajabu katika utekelezaji wa bajeti ya sekta, na sehemu ya kutofanya vizuri inaweza kuelezwa na utoaji mdogo wa fedha za wafadhili.

**Mtazamo wa karibu wa hatari zinozoweza kuathiri usimamizi wa fedha unaonyesha kwamba hatari hizi zipo katika pande zote mbili za mapato na matumizi.** Kwa upande wa mapato, hatari kubwa iliyo dhahiri ni kuanguka kwa mapato ya ushuru, kama asilimia ya Pato la Taifa. Upungufu katika mapato yanayotokana na ukusanyaji wa ushuru ulionekana kwanza katika mwaka wa fedha wa 2009 wakati ambapo ukuaji wa uchumi wa nchi ulianza kudhoofika polepole. Hasa, kushuka kwa ukuaji wa matumizi ya bidhaa nchini kulipunguza ukusanyaji wa Kodi ya Nyongeza ya Thamani (VAT). Ikiwa upungufu huu utaendelea, ongezeko la pengo katika bajetikutadhoofisha kudhibiti kwa deni la taifa.

**Hata hivyo, kunamatumaini tukizingatia kwamba iwapo baadhi ya marekebisho**—Kama yatatekelezwa—yanaweza kusaidia kuongeza mapato ya nchi.Baadhi ya marekebisho hayani kama kuziba njia za kupoteza pesa(kwa mfano katika usimamizi wa kodi na kuboresha viwango vya kufuata). Hata hivyo, ni lazima pia kukumbuka kwamba utegemezi mkubwa kwa kodi ya mapato kunadhoofisha motisha ya akiba na uwekezaji, iliyo pia na umuhimu sawa katika uchumi na kwa ajili ya usimamizi wa fedha.

**Kwa upande wa matumizi, shinikizo kuu la matumizi latokana na madai ya mishahara.** Madai kutoka mashirika mbalimbali ya sekta ya umma (hospitali, shule, vyuo vikuu, wafanyikazi wa serikali, bunge la kitaifa na wafanyikazi wa kaunti)ya nyongeza za mishahara na nafasi zaidi za ajira (kwa mfano, kuongeza idadi ya walimu kwa kuajiri wapya) kunaleta shinikizo za kifedha. La ajabu ni kwamba, Kenya imepiga hatua kubwa katika kupunguza mishahara ya wafanyikazi wa umma katika muongo uliopita: sekta ya umma kama asilimia ya Pato la Taifailishuka kutoka asilimia 8.5 mwaka wa 2000 hadi chini ya asilimia 7 katika mwaka wa fedha wa 2011/12. Hata hivyo, kuongezeka kwamahitaji yasiyokoma ya sasa (yaani tangu 2011) kumegeuza mwenendo huu wa zamani wa maendeleo (Tazama Sehemu 3.3 kwa uchambuzi wa kina wa madai ya mishahara).

**Wakati huohuo, matumizi makubwa yasiyokuwa na uhakika yatokana na ugatuzi unaoendelea.** Shinikizo lingine la matumizi linatokana na matumizi ya ziada yanayohitajika kufadhili msaada wa serikali za kaunti, yaani taasisi mpya, mahitaji ya wafanyakazi, utendaji, matunzo, vifaa, magari, majengo, na kadhalika.

**Kama serikali itafaulu kudhibiti hatari zinazokumba fedha, itahitajika kuchukua mbinu zilizochunguzwa kwa makini, ikijenga juu ya mafanikio ya awali.** Kwa mfano, ingawa serikali ina

nafasi ya matumizi ya maendeleo, lazima pia itie usawa gharama kubwa ya kukopa, pamoja na ongezeko la ghafla la riba ambalo linaweza kudhoofisha kukopa kwa sekta ya kibinafsi. Aidha, mbinu nyingine ni kuletahatua zenye nguvu na juhudi zinazoweza kuboresha tija na ufanisi wa matumizi—mkakati unaoweza kuletanafasi kubwa zaidi ya usimamiza mwema wa fedha katika nchi bila gharama ya kukopa.

**Ni mafunzo yapi tunayoweza kupata kuhusu tabia bora za matumizi, na hasa kwa ajili ya ubora, ufanisi, na matokeo mema kwa Kenya?** Funzo moja lenye fora kutoka kwa Uchambuzi wa Matumizi ya Umma (Public Expenditure Review) ni kwamba matumizi yanaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa bila ya kuhatarisha matokeo ya maendeleo. Matokeo yanaweza kuboreshwa iwapo matumizi yatafanywa yawe na ufanisi zaidi. Hili ni funzo muhimu kwa serikali za kitaifa na za kaunti, na kwa sekta mbalimbali. Uchambuzi wa sekta ya elimu, kwa mfano, unaonyesha kwamba elimu ya bure ya masomo ya msingi iliongeza kwa kiasi kikubwa usambazaji wa pembejeo za elimu, lakini si matokeo ya elimu. Uchambuzi pia unaonyesha kwamba matokeo ya elimu yanaweza kuboreshwa na kiwango sawa cha matumizi iwapo walimu watatumia muda zaidi darasani. Hii ina maanisha kwamba sekta hii—ambayo inatumia karibu theluthi ya matumizi yote ya kawaida ya Kenya—ina uwezo wa kufikia matokeo bora ikitumia kiwango sawa cha matumizi, asilimia 6.4 ya Pato la Taifa.

# UTANGULIZI

**Hili ni toleo lililorahisishwa la Uchambuzi wa Matumizi ya Umma (PER), linaloweza kuambatanishwa na Ripoti ya Kina ya Uchambuzi wa Matumizi ya Umma (CPER–2013).** Toleo hili linaonyesha maendeleo ya hivi karibuni katika sera ya fedha na mwenendo wa mgawo wa bajeti na utekelezaji. Tofauti kati ya ripoti hii na ile ya kina ni kwamba ripoti hio inachukua mtazamo wa miaka mitatu, bali toleo lililorahisishwa linamulika maendeleo katika usimamizi wa fedha katika muongo uliopita pamoja na kutambuamuhtasari wa mambo muhimu ya kisekta. Pia, inatoa uchunguzi wa kisayansi wa ufanisi wa matumizi katika sekta ya elimu ambayo inachukua asilimia 30 ya jumla ya matumizi ya kawaida na karibu robo tatu ya bajeti ya sekta ya rasilimali za kibinadamu, na kwa wastani, asilimia 6.4 ya Pato la Taifa.Toleo hililinabainisha jumbe nnemuhimu kama ifuatavyo:

**Kenya imekuwa namiaka kumi ya mafanikio ya usimamizi wa sera za fedha.** Serikali imekuwa na mafanikio mara tatu ya kupunguza mzigo wa deni la kitaifa na kupanua sana matumizi ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa yameleta manufaa kwa sekta ya miundo misingi. Mafanikio haya yanaonekana vyema zaidi katika muktadha wa mgogoro wa fedha wa 2010/11.

**Kenya bado inaweza kulipa madeni yake.** Kenya haina haja ya kupanua pengo lake la deni wala kuchukuahatuaza dharura sana katika uimarishaji wakifedha. Kiasi cha matumizi cha sasa kinatosha kushughulikia mahitaji ya maendeleo muhimu ikiwa rasilimali zitatumika kwa ufanisi zaidi. Katika viwango vya makadirio ya ukuaji waasilimia 5, Kenya yaweza kudumisha pengo la matumizi ya msingi la asilimia 2 ili kurudisha viwango vya madeni ya nyuma hadi asilimia 40 ifikapo mwaka 2015 (kutoka asilimia 44 mwaka 2012).

**Viwango vya sasa vya Kenya vya matumizi ya umma (karibu asilimia 30 ya Pato la Taifa) na muundo wa sekta kimatumizi viko sawa.** Katika siku za usoni, changamoto kuu ni za aina mbili: (i) mpito kwa mfumo wa ugatuzi wa serikali na mkazo wa kupanua matumizi ya sasa, (ii) ubora/ ufanisi wa matumizi kwajumla (jambo lililo wazi sana katika sekta ya elimu maalum kama kuzingatia mambo muhimu).

**Mazoea makubwa ya pesa za wafadhili zilizopeanwa nje ya bajeti yanadhoofisha kipaumbele cha kimikakati na upana wa bajeti.** Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za wafadhili mara nyingi

huwa changamoto, hata chini ya mfumo wa serikali kuu, na utakuwa mgumu zaidi pindi matumizi yatakapokabidhiwa serikali za kaunti 47. Aidha, utoaji mdogo wa pesa zawafadhili na taratibu za ununuzi zisizokuwa na ufanisi zinazorotesha utekelezaji wa bajeti.

**Ripoti hii imepangwa kama ifuatavyo: Sehemu ya Kwanza inaangazia maendeleo ya sera za kifedha katika miaka kumi iliyopita.** Sehemu ya Pili inaonyesha mambo muhimu ya sekta pamoja na uchambuzi wa bajeti na viwango vya utekelezaji vya sekta mbalimbali na uainishaji wa kiuchumi; sehemu hii pia inachambuautendajikazi wa mapato. Sehemu ya Tatuinatathmini shinikizoza kifedha zinazojitokeza katika kipindi cha muda wa wastani. Sehemu ya Nne inalenga sekta ya elimu na kuwasilisha matokeo ya ripoti ya utafiti wa matumizi ya umma na huduma (PETS + +) iliyofanywa hivi karibuni. Sehemu ya Tano inatoa muhtasariwa kuhitimisha.

Sura ya 1

# MUONGO WA MAENDELEO: FAIDA MARA TATU

1.1 **Serikali imepata faida mara tatu katika usimamizi wa fedha.** Kwanza, sehemu ya matumizi ya maendeleo imeongezeka kutoka asilimia 4 hadi asilimia 10 ya Pato la Taifa wakati ambapo sehemu ya matumizi ya kawaida ilipungua hatua kwa hatua kutoka asilimia 24 mwanzoni mwa muongo na kuimarishwa katika wastani wa asilimia 20 ya Pato la Taifa. Pili, madeni yalipungua kutoka asilimia 54 hadi asilimia 39 ya Pato la Taifa. Ingawa deni la taifa limeongezeka hivi karibuni, bado lilikuwa katika mipaka inayokubalika ya asilimia 44 ya Pato la Taifa mwakani 2012. Tatu, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo umeongezeka kwa asilimia 15 hadi asilimia 75.


1.2 **Mafanikio haya yalipatikana kupitia sera mbalimbali ikiwemo:** Kudhibiti ongezeko la madai ya mishahara ya wafanyikazi wa umma, kuweka kiwango kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida cha jumlaya asilimia 20 ya Pato la Taifa, ongezeko la fedha za nje, na viwango vya juu vya kukopa pesa ndani ya nchi. Fauka ya hayo, kumekuwa na kubadilisha kwa kimakusudi kwa njia ya serikali kupata pesa nchni kutoka kwa matumizi ya bili za hazina za siku 91 hadi dhamana za serikali za muda mrefu, ili serikali iwe na muda mrefu wa kulipa na pia kuambatana na uwekezaji ambao utazaa matunda baada ya muda mrefu. Sehemu hii inafuatilia shughuli za sera zinazoegemeza mafanikio haya na kumalizia na uchambuzi wa hivi karibuni wa maendeleo katika sera za kifedha.

## Matumizi ya kimaendeleo yameongezeka kwa njia zote

1.3 **Matumizi ya kimaendeleo kama sehemu ya Pato la Taifa yameongezeka mara dufu tangu mwaka wa 2005 na kufikia takriban theluthi moja ya jumla ya matumizi yote katika mwaka wa 2012.** Kati ya mwaka wa 2003 na 2011, kiwango cha ukuaji cha miradi ya maendeleo

kilikuwa asilimia 26 kikilinganishwa na 4.8 ya mishahara na 9.3 ya utendaji na gharama za kukimu (angalia Kielelezo 1). Matumizi ya kimaendeleo yameongezeka mara 14 kutoka kiasi kidogo cha bilioni 16 mwaka 2003 hadi bilioni 230 mwaka 2011. Sehemu tofauti za matumizi ya maendeleo pia zimeboreshwa. Matumizi ya bidhaa za mtaji yameongezeka kutoka asilimia 40 hadi takriban asilimia 60.[1] Mgawo wa kima cha chini kwa matumizi ya maendeleo sasaimetia nanga katika sheria ya usimamizi wa fedha za umma uliopitishwa mwaka 2012, uliowekwa katika kiwango cha chini cha asilimia 30 ya jumla ya matumizi.

**Kielelezo 1: Kupunguza pengo kati ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo**




*Chanzo: Ukadirifu wa Wafanyikazi wa Benki ya Dunia (World Bank )uliotumia data kutoka kwa Hazina ya Taifa*


**1.4** **Ili kufanikisha maelekezo haya ya matumizi, serikali ilitia kikomo ongezeko la matumizi ya kawaida.** Serikali imeendeleza matumizi ya kawaida katika wastani waasilimia 20 ya Pato la Taifa katika miaka kumi iliyopita na yanakadiriwa kubaki katika kiwango hicho hicho katika kipindi cha wastani (Kielelezo 1). Matumizi yautendaji nakukimuni sehemu kubwa ya matumizi ya kawaida, takriban asilimia 49 na huchukua asilimia 45 ya mapato ya kawaida. Serikali inakusudia kupunguza uwiano wa matumizi haya kwa mapato ya kawaida uwe asilimia 40 katika kipindi cha wastani.

**1.5** **Ongozeko la matumizi ya maendeleo limetumiwa kufadhili miundo misingi.** Kielelezo 2 kinaonyesha mabadiliko katika vipaumbele vya sektanakulinganishwa kwa matumizi ya wastani ya vipindi viwili, 2002-2005 na 2006-2009. Bajeti ya miundo misingi imeongezeka mara tatu namgawo wa sekta katika jumla ya matumizi kuongezeka kutoka asilimia 14

[1] *Bajeti ya maendeleo ya vitengo vyenye gharama za aina ya kawaida nazinazotegemea sana wafadhili.*

hadi 21, ikiwa ya pili baada ya maendeleo ya rasilimali ambayo inachukua asilimia 29 ya jumla ya matumizi ya sekta. Mgawo wasekta ya utawala imepungua kutoka asilimia 20 hadi 14 sawa na ile ya utawala wa umma. Sekta hizi nne (kati ya nane) zinachukua asilimia 80 ya bajeti, tazama kiambatanisho cha 2. Sekta ya miundo misingi inashughulikia barabara na kazi za umma, nishati, usafiri na wizara ya serikali za mitaa. Katika sekta hii, wastani waasilimia 77 ya bajjeti inakwenda kwa barabara na nishati.

**Kielelezo 2: Miundo misingi na maendeleo ya rasilimali inachukua zaidi ya asilimia 50 ya jumla ya bajeti ya sekta**





*Chanzo: Ukadirifu wa Wafanyikazi kwa kutumia akaunti za matumizi za Ofisi ya Ukaguzi (KENAO) na makadirio yaliyochapishwa ya Serikali ya Kenya*

1.6 **Wafadhili hukidhi takriban asilimia 33 ya matumizi ya maendeleo,** hasa miundo misingi (asilimia 3 ya Pato la Taifa) amabayo inapungua hadi asilimia 1.5 ya Pato la Taifa ikirekebishwa kuzingatia utoaji halisi. Sehemu ya fedha za wafadhili inayotengewa miundo misingiimeongezeka kwa muda kutoka takriban asilimia 42 mwaka wa 2005/06 hadi 56 mwaka wa 2011/12. Kipindi hicho kimeshuhudia kupungua kwa fedha za wafadhili zilizotengewa sekta ya maendeleo ya rasilimali kutoka asilimia 25 mwaka 2005/06 hadi takriban asilimia 14 katika miaka ya hivi karibuni.[2] Maji na Mazingira na sekta ya hifadhi ya jamii pia zimefaidika kutokana na ongozeko la fedha kutoka kwa wafadhili ingawa sehemu ya rasilimali iliyotengewa sekta ya hifadhi ya jamii hutofautiana mwaka kwa mwaka na hasa huwa juu katika miaka ya ukame. Hata hivyo, wastani wa kiwango cha utoaji wa fedha za wafadhili hutofautina kati ya asilimia 45 na 50 ambayo hupunguza sehemu halisi ya wafadhilikatika bajeti ya maendeleo kutoka asilimia 30 hadi takriban asilimia 15 au asilimia 1.5 ya Pato la Taifa. Msaada wa fadhili (katika bajeti) na sehemu ya serikali/ na ya wafadhili zimeonyeshwa katika Kielelezo 3.

1.7 **Kuna sehemu kubwa ya fedha za wafadhili zilizo nje ya bajeti. Uchambuzi hadi sasa unalenga fedha zilizoko kwenye bajeti,** lakini kuna kiwango kikubwa cha miradi inayoelekezwa nje ya bajeti. Wafadhili kutoka nchi za Marekani na China bado wanapendelea kutekeleza mipango yao nje ya mifumo ya serikali; vile vile, wafadhilli wapya, hasa

[2] *Kushuka huku kunaweza kuwa kumehusishwa na uondoaji wa msaada wa wafadhili kutoka kwa mfumo wa elimu ya bure.*


**Kielelezo 3: Wafadhili wanakidhi takriban asilimia 33 ya matumizi ya maendeleo, hasa miundo misingi**




*Chanzo: Makadirio ya serikalii yaliyochapishwa (miaka mbalimbali)*

wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGOs), kwakawaida huchagua kutekeleza miradi yao moja kwa moja kuliko kupitia utawala wa serikali. Fedha hizo zinapozingatiwa, umuhimu wa fedha za nje unaongezeka kwa wastani wa asilimia 4.2 ya muongo uliopita (Kielelezo 4). Sekta ya afya inatoa mfano mzuri wa fedha za wafadhili zilizo nje ya bajeti: makadirio yanaonyesha kwamba katika mwaka wa 2009/10 wafadhili katika sekta ya afya walitumia zaidi ya shilingi bilioni 50 nje ya mifumo ya bajeti; angalia maelezo ya Sehemu 2.3 (Mambo muhimu ya sekta ya afya).

**Kielelezo 4: Kupungua kwa fedha za wafadhili kama sehemu ya jumla ya bajeti**




*Chanzo: Takwimu kutoka Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD)*

Sura ya 2

# MAMBO MUHIMU YA SEKTA[1]

## Sekta ya Miundo Misingi

2.1 **Katika muongo uliopita, Kenya imefanya maendeleo ya ajabu katika uwekezaji wa miundo misingi hasa katika kufikia malengo yake ya Ruwaza ya Kenya 2030 (Kenya Vision 2030).** Maendeleo haya yamejitokeza kupitia mabadiliko yaliyoonekana katika matumizi ya maendeleo ambayo yameshuhudia kuongezeka kwa matumizi ya fedha hasa kwa ajili ya maendeleo ya miundo misingi nchini kote. Hata hivyo, pengo la miundo misingi bado lipo na kiwango cha juu cha uwekezaji kitahitajika kuwa na uimarishajiili kuziba pengo hilo.

2.2 **Katika kipindi cha 2009/10 hadi 2011/12, serikali ilitenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya miundo misingi katika bajeti zote—ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo.** Jumla ya bajeti ya miundo misingi iliongezeka kutoka shilingi bilioni 146.3 hadi shilingi bilioni 217.5 katika kipindi hiki. Matumizi ya maendeleo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 106.8mwaka 2009/10 hadi shilingi bilioni 161.9 mwaka 2011/12. Matumizi halisi yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 80.6 katika mwaka 2009/10 hadi shilingi bilioni 128.7 mwaka 2011/12. Ongezeko katika mgawowa matumizi ni sawasawa na matakwaya serikali na pia utambuzi kwamba miundo misingi ya nchi ni msingi wa kufikia malengo ya Ruwaza ya Kenya ya 2030. Hata hivyo, sehemu kubwa ya bajeti katika sekta yatoka kwawafadhili.

2.3 **Jumla ya matumizi ya miundo misingiilikuwa katika wastani waasilimia 10 ya Pato la Taifa katika kipindi hiki, na sekta ndogo za barabara na nishati zilichangia asilimia 80 ya jumla ya bajeti ya miundo misingi (Kielelezo 5).** Sekta ya barabara inapata sehemu kubwa


[1] *Sekta ya elimu imeangaziwa katika Sehemu ya Nne.*

ya jumla ya bajeti ya miundo misingi. Uwekezaji katika sekta hii ndogo uliongezeka kwa asilimia 29 kutoka shilingi bilioni 86 mwaka 2009/10 hadi shilingi bilioni 110.9 mwaka 2011/12 (Kielelezo 6).

**2.4** **Jumla ya bajeti katika sekta ndogo ya nishati imeongezeka mno kwa asilimia zaidi ya 70nakuwa shilingi bilioni 57.5 mwaka 2011/12 kutoka shilingi bilioni 35.5 mwaka 2009/10.** Bajeti ya maendeleo ilichangia sehemu kubwa zaidi—asilimia 95 kwa wastani katika taifa (Kielelezo 7). Matumizi kwaupatikanaji wa mali zisizo za kifedha yalikuwa katika wastani wa asilimia 49 na malipo ya wafanyikazi na matumizi ya bidhaa na huduma yalipata migawo midogo kwa wakati huu, na hii inaelezea mwelekeo wa uwekezaji kati katika mtaji.

**2.5** **Asilimia 14 pekee ya jumla ya barabara ilikuwa nalami katika kipindi cha 2000-2010 (Kielelezo 8).** Jumla ya mtandao wa barabara nchini ni kilomita 160,886; kati ya hizo ni kilomita 8,880 tu zilizo za lami. Barabara zilizobaki hazina lami (hii imeenea kote nchini). Hii inaonyesha kwamba sehemu kubwa ya nchi haijanufaika ilihali sehemu hizo zina uwezo mkubwa wa kuendeleza uchumi wa kitaifa. Hata hivyo, uwezo huu haujatumiwa. Kwa hiyo, ongezeko la hivi karibuni katika viwango vya uwekezaji katika maendeleo ya miundo misingi, hasa katika sekta ndogo ya barabara lazima yaonyeshe kuongezeka kwa maili ya barabara zenye lami.

**Kielelezo 5: Barabara na nishati zinachangia asilimia 80 ya jumla ya matumizi ya miundo misingi**





*Chanzo: Makadirio ya wafanyikazi kutumia ripoti za Sekta za Nishati, Miundo Misingi na Mawasiliano na Teknolojia*

**Kielelezo 6: Uwekelezaji katika barabara hasa umelenga maendeleo**





*Chanzo: Ripoti ya sekta ya mawasiliano na teknolojia*

### Kielelezo 7: Uwekezaji katika sekta ndogo ya kawi umelenga hasa usambazaji wa umeme kote nchini




Chanzo: Wizara ya Kawi

### Kielelezo 8: Kulinganishwa kwa viashiria vya miundo misingi nchini




Chanzo: Benki ya Dunia, Viashirio vya maendeleo ya dunia

2.6 **Aidha, mahitaji ya Kenya ya nishati yanapita kadiri ya upatikanaji wake.** Uzalishaji wa nishati za kipimo cha tani elfu za mafuta upo nyuma ukilinganishwa na nchi za Afrika (Kielelezo 8). Japo mahitaji ya umeme yanazidi kuongezeka, niasilimia 29 tu ya idadi ya watu waliokuwa wamefikiwa na umeme mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 15 mwaka 2004. Kumbukumbu na historia ya mahitaji ya umeme na utabiri wa mahitaji ya umeme unaonyesha ongezeko thabiti la mahitaji ya umeme (inakadiriwa kuwa asilimia 8 kwa mwaka)—tazama Jedwali 1 ingawa kuna kuimarika kwa ongezeko la mahitaji ya umeme, uwezo wa kutosha uliopo kukidhi mahitaji haya bado haujaimarishwa.

**Jedwali 1: Takwimu za mahitaji na matumizi**

| | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nishati iliyotengenezwa (GWh) | 5,347 | 5,697 | 6,169 | 6,385 | 6,489 | 6,692 | 7,303 | 7,670 |
| Nishati iliyouzwa (GWh) | 4,379 | 4,580 | 5,065 | 5,322 | 5,432 | 5,624 | 6,123 | 6,341 |
| Mahitaji ya kilele (MW) | 899 | 920 | 987 | 1,044 | 1,072 | 1,107 | 1,194 | 1,236 |
| Idadi ya watumiaji | 735,144 | 802,249 | 924,329 | 1,060,383 | 1,267,198 | 1,463,639 | 1,753,348 | 2,038,625 |

*Chanzo: Ripoti ya mwaka pamoja na taarifa za fedha, 2012 ya Kampuni ya Umeme ya Kenya*


## Sekta ya Maji

2.7 **Upatikanaji wamaji salama na yakuaminika ni pembejeo muhimu katika kupunguza umaskini na kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia na malengo ya Ruwaza 2030.** Lakini chakusikitisha ni kwamba hii ni moja ya sekta ambayo imekuwa namaendeleo madogo kabisa.Tathmini ya mafanikio katika mpango wakipindi chawastani cha kwanza inaonyesha kwamba kulikuwa na ongezeko la asilimia 2 kwa idadi ya nyumba za mijini na upatikanaji wa maji ya bomba ili kufikia asilimia 60 ikilinganishwa na asilimia 72 ya lengo la mwaka 2012. Uwiano wa nyumba na upatikanaji wa maji kutoka vyanzo vilivyolindwa ulipungua kutoka asilimia 49 mwaka 2010 hadi asilimia 45 mwaka 2012. Uhifadhi wa maji kwa kila mwananchi uliongezeka kidogo kutoka mita 4.6 za ujazo hadi 5.3. Hata hivyo, kiwango hiki nichini zaidi kuliko kusudio la 2012 la mita 16 za ujazo.

2.8 **Karibu nusu ya idadi ya Wakenya wanategemea maji yaliyo juu ya ardhi na theluthi mbili wanategemea vyoo vya kawaida.**[2] Mlingano unaonyesha kwamba ni asilimia 18 tu ya Wakenya wanaopata maji ya bomba, ikilinganishwa na asilimia 56 katika nchi za kipato cha kati (angalia Kielelezo 9). Upanuzi wa maji ya bomba haijaweza kufikia idadi ya watu inayoendelea kukua kwa kasimno. Ingawa upatikanaji wa maji ya bomba umeshuka zaidi katika muongo uliopita, upatikanaji wa maji ya vyanzo vya maji vilivyoboreshwa imeongezeka. Muundo sawa unaweza kuonekana katika upatikanaji wa usafi wa


[2] *Nambari katika sehemu hii ni za mwaka 2009 ili kuwezesha kulinganisha Kenya na nchi zingine.*

**Kielelezo 9: Asilimia 18 ya Wakenya wanapata maji ya bomba ikilinganishwa na asilimia 56 ya nchi za kipato cha kati**




*Chanzo: Benki ya Dunia, Ripoti ya Kuchunguza Miundo Misingi ya Afrika (AICD) 2010*

**Kielelezo 10: Upatikanaji wa maji katika kaunti**





*Chanzo: Kenya National Bureau of Statistics, 2010*

mazingira: asilimia 9 tu ya Wakenya wanaweza kupata matangi ya kukusanya taka za maji ikilinganishwa na asilimia 44 katika nchi za kipato cha kati. Chanzo kikuu cha usafi wa mazingira cha asilimia 64 ya wakenya ni vyoo vya kawaida. Karibu asilimia 18 ya Wakenya hawana usafi wa mazingira. Idadi hii inakaribiana na ile ya watu kutoka nchi za kipato

cha kati ambayo ni asilimia 15 (Kielelezo 9). Kwa nchi ambayo kiasi kikubwa nivijiji, utumizi wa vyoo vya kawaida inakubalika. Hata hivyo, viwango vya upatikanaji nivya maana zaidi wakati mgawanyiko kati ya mji, vijijini na mijini unazingatiwa.

**Kielelezo 11: Karibu robo tatu ya bajeti ya maji huenda katika huduma za usambazaji wa maji**




*Chanzo: Matumizi ya Mfumo wa Muda/Kipindi cha Kati (MTEF)–Sekta ya Mazingira, Maji na Makazi (2012)*

2.9 **Kama huduma nyingine za kimsingi, upatikanaji wa maji unabakia umejilimbikiza katika maeneo fulani.** Kielelezo 10 kinaonyesha upatikanaji wa maji yaliyoboreshwa katika kaunti. Ni wazi kwamba kaunti chache tu ndizo (karibu 4 kati ya 47) zimefikia lengo la Maendeleo ya Milenia. Kaunti zote zingine nchini zipo chini ya lengo hili lakini tofauti katika upatikanaji wa maji ni ya kustaajabisha; katika kaunti 6, upatikanaji wa maji yaliyoboreshwa ni chini ya asilimia 40, karibu nusu ya kaunti zinazoongoza. Kwa hivyo, uwekezaji mkubwa watakiwa kupanua upatikanaji wa maji.

2.10 **Sekta ya maji inachukua karibu asilimia 3.5 ya jumla ya matumizi ya serikali ikiwakilisha asilimia 0.7 ya Pato la Taifa (Jedwali 2).** Karibu robo tatu ya bajeti ya sekta ya maji huenda kwa huduma ya ugavi wa maji wakati sehemu iliyobaki ikigawanywa kati ya programu nyingine zote (angalia Kielelezo 11). Katika kipindi cha 2009/10 hadi 2011/12, sekta hii


**Jedwali 2: Matumizi kwa ajili ya sekta ya maji ikilinganishwa na Jumla ya Pato la Taifa na Jumla ya matumizi ya umma**

| | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 |
|---|---|---|---|
| Jumla ya Bajeti ya Wizara ya Maji | 27,789 | 38,613 | 36,215 |
| Jumla ya Matumizi ya Serikali | 789,361 | 922,563 | 1,165,532 |
| Matumizi kwa Maji,% ya Jumla ya Matumizi ya Serikali | 3.5 | 4.2 | 3.1 |
| Jumla ya Pato la Taifa, bei za sasa | 2,366,984 | 2,549,825 | 3,024,782 |
| Matumizi kwa Usambazaji wa Maji, % Jumla ya Pato la Taifa | 0.6 | 0.7 | 0.7 |

*Chanzo: Matumizi ya Mfumo wa Muda/Kipindi cha Kati (MTEF) – Sekta ya Mazingira, Maji na Makazi (2012)*

ilishuhudia mabadiliko makubwa ya sera na marekebisho ambayo yalikuwa yanalenga kuhakikisha kwa kanuni husika na utoaji wa kutosha wa huduma.

**Kielelezo 12: Gawo la matumizi ya serikali naya wafadhili katika sekta ya maji**




*Chanzo: Matumizi ya Mfumo wa Muda/Kipindi cha Kati (MTEF) – Sekta ya Mazingira, Maji na Makazi (2012)*

**2.11** **Tofauti na sekta nyingine, robo tatu ya bajeti ya sekta hii ni ya maendeleo.** Ingawa sehemu kubwa ya matumizi ya maendeleo ni ya muhimu, inasababisha changamoto tofauti kwa sekta: (i) inafanya baadhi ya programu kutokuwa na utendajikazi wa kutosha kutokana na kupunguzwa kwa bajeti ambayo hutolewa kutoka kwa matumizi ya maendeleo, na (ii) kucheleweshwa kwa kutoa fedha za wafadhili na hazina huathiri pakubwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Ni muhimu pia kutambua kwamba sekta hiiinategemea zaidi wafadhili na zaidi ya asilimia 40 ya matumizi hutoka kwa wafadhili na kiasi kidogo hutoka kwa sekta ya kibinafsi (Kielelezo 12). Hii inaonyesha kuwa sekta ya maji inaweza kudhuriwa kwa urahisi na ipo haja ya kutafuta njia za kuhamasisha fedha kutoka kwa sektaza kibinafsi za humu nchini.

**2.12** **Ili sekta itimiza malengo yake, kuna haja ya kukusanya rasilimali kupitia** (i) Ushirikiano wa umma na sekta binafsi (PPP), kwa kutumia taratibu na vyombo kama vile motisha wa kodi na udhibiti wa kuwezesha mazingira, mambo ambayo yangeweza kuvutia wawekezaji katika sekta binafsi, (ii) ufadhili wa vielelezo na sera kuwezesha makubaliano na umiliki ili kuongeza ufadhili wa sekta, na (iii) mpango wa uwekezaji katika sekta ya maji na katika miradi mbalimbali kwenye sekta hiyo mpango. Sekta ni lazima pia kuanzisha utaratibu wa bajeti/fedha ili kufuatilia na kutoa taarifa kwa mipango yote, kwa ushirikiano wa karibu na washirika wa maendeleo, Hazina ya Taifa na mashirika tekelezi.

## Sekta ya Afya


**2.13** **Sekta ya afya imepata mafanikio katika baadhi ya viashiria muhimu tangu uchambuzi wa matumizi ya umma yaliyopita.** Sekta imeweza kupunguza kiwango cha vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano kutoka watoto 83 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2008 hadi watoto 73 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2011. Vifo vya


**Jedwali 3: Mwelekeo wa viashiria muhimu vya afya**

| Kiashiria | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya kiwango cha uzazi (uzao kwa kila mwanamke) | 4.8 | 4.8 | 4.8 | 4.7 | 4.7 |
| Kiwango cha vifo vya watoto (kwa kila watoto 1,000 waliohai) | 56 | 53 | 52 | 50 | 48 |
| Kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5(Kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai) | 87 | 83 | 79 | 76 | 73 |
| Watoto chini ya mwaka 1waliochanjwa dhidi ya surua (%) | 80 | 90 | 88 | 86 | 87 |
| Uwiano ya wamama wanaojifungua(Kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai) | - | 490 | 488 | 473 | - |
| Watu wanaoishi na VVU/HIIV, 15-49 years old, % | 6.4 | 6.3 | 6.2 | 6.2 | 6.2 |
| Kiwango cha matukio ya HIV, 15-49 years old, % | 0.53 | 0.54 | 0.5 | 0.47 | 0.45 |
| Kiwango cha maambukizi ya kifua kikuu (kwa kila watu 100,000) | 317 | 309 | 291 | 288 | 291 |
| Kiwango cha maambukizi ya kifua kikuu (kila mwaka, kwa kila watu 100,000) | 347 | 332 | 312 | 298 | 288 |

*Chanzo: Idara ya Afya, 2012*

**Kielelezo 13: Kenya inaendelea vyemaikilinganishwa na nchi zingine tukiangazia wauguzi na vitanda kwa kila watu 10,000**





*Chanzo: Data kutoka Shirika la Afya Duniani ( WHO), 2012 na Utafiti wa Uchumi, 2012*
*(*data ya Ghana ni ya mwaka 2009, **Kenya ni ya mwaka 20100; data ya nchi zingine ni za mwaka 2008)*

watoto wachanga vimepungua kutoka 53 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai hadi 48 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai katika kipindi hicho. Sekta pia imeshuhudia kuongezeka kwa utoaji wa chanjo kwa watoto chini ya mwaka mmoja kutoka asilimia 71 mwaka 2008 hadi asilimia 77 mwaka 2011. Matukio na maambukizi ya kifua kikuu na Virusi Vya Ukimwi pia vilishuka wakati wa kipindi hiki (Jedwali 3).


**Kielelezo 14: Wanaochangia mzigo wa magonjwa**




*Chanzo: Ripoti ya Sera ya Afya ya Kitaifa; Wizara ya Huduma za Afya na Usafi na Afya ya Umma, 2011*

**2.14 Kwa ajili ya mafanikio hayo, Kenya inalingana vyema nanchi zingine za Kiafrika.** Kwa mfano, Wakenya 10,000 wanatibiwa na 8.3 ya wauguzi ikilinganishwa na 4.2 nchini Senegali na 10.5 nchini Ghana. Vile vile, idadi ya vitanda hospitalini vinavyopatikana kwa Wakenya 10,000 imeongezeka kutoka 9 mwaka 2010 hadi 13 mwaka 2011, ambayo inalinganishwa

**Kielelezo 15: Watoto waliochanjwa kikamilifu kwa kaunti (Miezi 12-23)**





*Chanzo: Utafiti wa Bajeti za Nyumbani (KIHBS), 2005/06*

na vitanda 9 kwa kila Waghana 10,000 na ni vyema kuliko Uganda ambapo uwiano ni vitanda 4 kwa kila watu 10,000 (Kielelezo 13).

2.15 **Hata hivyo, sekta bado inakabiliana na changamoto zisizokoma.** Changamoto muhimu kati ya hizi nikiwango cha juu cha vifo vya akina mama wanaojifungua/ waliojifungua na mzigo wa kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Vifo vya akina mama wanaojifungua/ waliojifungua imebaki juu na bado iko zaidi ya viwango vya mwaka 2003. Mafanikio katika sekta ni kushuka kidogo kwa vifo kutoka 490 mwaka 2008 hadi vifo 473 mwaka 2010. Watoto waliozalishwa na wauguzi wa afya wenye ujuzi ulipungua kutoka asilimia 51 mwaka 2007 hadi asilimia 43 mwaka 2010/11, licha ya ufadhili mkubwa katika programu hizi. Sekta pia inakabiliwa na mizigo ya aina mbili, ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, kama inavyonekana katika Kielelezo 14.

**Kielelezo 16: Matumizi ya serikali katika sekta ya afya kama asilimia ya jumla ya bajeti**





*Chanzo: Akaunti za matumizi, Ofisi ya Kitaifa ya Ukaguzi ya Kenya ( KENAO ), NHA, Idara ya Afya–Mfumo wa Matumizi ya Kipindi cha Kati (MTEF), 2010-2012*

2.16 **Sekta hii pia inakabiliwa na tofauti kubwa za kijiografia katika upatikanaji wa huduma za afya.** Katika Kielelezo 15, upatikanaji wachanjo unatumika kama mfano wakuonyesha tofauti hizi zakijiografia lakini ni lazima ieleweke kwamba hali hiyo inaigwa katika upatikanaji wa huduma nyingine za afya. Kielelezo kinaonyesha kuwa katika Kaunti ya Nyeri, watoto wote wenye umri wa miezi 12-23 wamechanjwa kikamilifu ikilinganishwa na nchini ya asilimia 10 ya watoto katika Kaunti ya Mandera. Mfano huu unaonyesha kwamba hata katika maeneo ambayo Kenya imefanya vizuri na kutimiza malengo ya kitaifa, kuna tofauti za kustaajabisha za kimaeneo katika upatikanaji wa huduma za afya. Tofauti hizikatika upatikanaji wa huduma zinatakikana kuarifu vipaumbele vya serikali za kaunti hasa sasa wakati ambapo matumizi katika sekta yamekabidhiwa kikamilifu kwa kaunti, ili kutoa fursa ya kuziba mapengo yaliyopo.

2.17 **Sehemu ya matumizi ya afya katika bajeti ya serikali imeongezeka kutoka asilimia 5 hadi asilimia 7.8, ambayo kihalisi niongezeko la asilimia 2.8 (Kielelezo 16).** Katika thamani


**Kielelezo 17: Japo sehemu kubwa ya fedha za wafadhili kuelekezwa nje ya mifumo ya serikali, nyumba nchini bado zina mzigo mkubwa wa huduma za afya**




*Chanzo: Akaunti za Taifa 2009/10, Bajeti Mwigo (Shadow Budget) 2009/10 na Msaada wa washirika wa Maendeleo ya Kenya (Development Partners Assistance to Kenya-DPAK), 2011*

bayana, matumizi ya serikali ya afya yameongezeka mno katika miaka iliyopita kutoka shilingi bilioni 38 mwaka 2009/10 hadi shilingi bilioni 59 mwaka 2011/12. Matumizi ya fedha kutoka kwa wafadhili pia imebaki juu, kufidia kupungua kwa matumizi ya nyumbani.

**Kielelezo 18: Asilimia 40 ya matumizi ya sekta ya afya inatumiwa kwa mishahara**





*Chanzo: Makadirio yaliyochapishwa, akaunti za matumiz (KENAO)*

2.18 **Matumizi ya afya ya umma yanakadiriwa kuwa dola za Marekani 19 kwa kila mwananchi.** Kwa ujumla, hata pamoja nakuongezeka kwa mgawowa sekta, matumizi kwa kila mwananchi kwa sasa ni dola za Marekani 19.2 kwa kila mwananchi. Jumla ya matumizi bado yako chinikwa sababu sasa ni dola za marekani 42 kwa kila mwananchi ikilinganishwa na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya dola za marekani 54 kwa kila mwananchi. Licha ya matumizi ya

serikali, sekta ya afya inafurahia sehemu kubwa ya fedha za wafadhili lakini nyumba nchni hubeba mzigo mzito. Jumla ya matumizi katika sekta ya afya inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 100, ambapo matumizi ya umma ni karibu asilimia 30, matumizi ya wafadhili inakadiriwa kuwa asilimia 27 na masalio ya karibu asilimia 43 ni matumizi ya afya kwa nyumba nchini.

**Kielelezo 19: Wastani wa mgawo wa matumizi ya afya kwa ajili ya tiba na kinga haijabadilika**




*Chanzo: Makadiri yaliyo chapishwa na Akaunti za matumizi (KENAO)*

**2.19 Sehemu kubwa ya matumizi ya wafadhili katika sekta ni nje ya bajeti.** Ijapokuwa sekta inafurahia fedha za kutosha kutoka kwa wafadhili (ilikadiriwa kuwa asilimia 50 mwaka 2010), kuelekezwa kwa fedha nje ya mifumo ya serikali kunatoa changamoto tatu kuu kwa sekta: (i) kunadhoofisha kipaumbele katika sekta kimikakati, (ii) huathiri uhakika wa rasilimali, na (iii) kunapunguza uwazi na uwajibikaji, kwa mfano, kunaweza kusababisha mahesabu tofautitofauti kwa ajili ya matumizi ya fedha, angalia Kielelezo 17.

**2.20 Matumizi kwa ajili ya miradi ya majengo/ mitambo katika sekta ya afya bado yako chini, karibu asilimia 14 ya jumla ya bajetilicha ya kuwepo kwa upungufu wa miundo misingi katika sekta.** Robo tatu ya matumizi katika sekta ya afya ni ya kawaida kiasili, na ingawa sehemu ya matumizi ya maendeleo imeongezeka katika miaka ya hivi karibuni, bado ni ndogo karibu asilimia 14 ya bajeti ya sekta (Kielelezo 18). Aidha, mgawo kati ya afya ya tiba na ya afya ya kingahaujabadilika licha ya ahadi ya kuongeza fedha kwa ajili ya afya ya kukinga magonjwa (angalia Kielelezo 19). Kwa mfano, misaada kwa hospitali mbili za rufaa (Moi na Kenyatta) zilikuwa na wastani wa asilimia 14 ya jumla ya bajeti ya afya katika miaka 2002-2010.


## Sekta ya Kilimo na Maendeleo ya Vijijini

**2.21 Sekta ya kilimonamaendeleo ya vijijini husaidia pakubwakatika ukuaji wa uchumi wa Kenya na inasalia kuwa njia moja muhimu ya kujikimu kimaisha kwa Wakenya wengi.** Sekta hii imetambuliwa kama moja ya sekta sita muhimu katika kutimiza asilimia 10 ya

ukuaji wa uchumi kulingana na malengo ya Ruwaza 2030. Katika mwaka 2011, sekta hii ilichangia moja kwa moja asilimia 24.5 ya Pato la Taifa lenye thamani ya shilingi bilioni 741. Sekta hii pia huchangia takriban asilimia 27 ya Pato la Taifa kupitia uhusiano na sekta ya viwanda, usambazaji na huduma nyingine kuhusika.


2.22 **Nchini Kenya, ongezeko la thamani kwa kila mfanyakazi katika kilimo imekuwa ikipungua tangu uchumi uwe huria katika miaka ya 1980 chini ya programu za kurekebisha miundo (Structural Adjustment programmes).** Hata hivyo, bado iko juu zaidi ya wastani wanchi za Kiafrika zinazoendelea kiuchumizilizo kusini mwa jangwa la Sahara na nchi za kipato cha chini. Ardhi katika maeneo ya uwezo wa wastani na pamoja na ardhikavu (ASALs) bado hazijatumiwa vilivyo katika uzalishaji wa kilimo. Ardhi ya kilimo mara nyingi pia haijatumika vilivyo na wakulima wadogo wakitumia tu asilimia 60 ya ardhi yao kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo.

**Kielelezo 20: Mgawo wa sekta ya kilimo, Shilingi bilioini (Bajeti ya maendeleo na ya kwaida)**




*Chanzo: Ripoti ya sekta ya kilimo, 2012*


**Kielelezo 21: Matumizi ya sekta ya hifadhi ya jamiikama asilimia ya jumla ya bajeti ya serikali 2009/10 - 2010/11**




*Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Kenya, Ripoti ya utafiti wa uchumi wa Taifa 2013*

2.23 **Viwango vya tija ya mazao mengi vipo chini nabaadhi ya thamani na mazao ya kilimo katika kipindi cha miaka mitano haijabadilika au hata imepungua.** Kitaifa, tija ya mazao ya viwanda kama vile kahawa na majani haijabadilika katika miongo miwili iliyopita. Hata hivyo, mazao mengine yameonyesha mchanganyiko wa matokeo. Maharagwe

**Kielelezo 22: Walengwa wa OP-CTP kwa kaunti kufikia Juni, 2012**




*Chanzo: Wizara ya Jinsia, Watoto na Maendeleo ya Jamii, 2012*

yamekuwa na ongezeko wakati ambapo mazao mengine kama kunde, mbaazi, gramu, nk. ilipungua. Vile vile, viwango vya uzalishaji wa bidhaa kutoka kwasamaki na mifugo vipo chini ya uwezo ya nchi. Misitu na tija ya miti imekuwa ikipungua wakati ambapo ongezeko la idadi ya watu limesababisha migogoro kuongezeka baina ya binadamu na wanyamapori. Tija katika sekta ya kilimo inakabiliwa na uhaba wa ugavi kutokana na uwezo mdogo wa kuhifadhi, ukosefu wa huduma baada ya mavuno na upatikanaji duni wa soko. Ruwaza ya Kenya2030 inatoa mwito wa juhudi zilizomakinika ili kudumisha masoko yaliyopo na kujenga mapya ili kuongeza nguvu ya sauti ya Kenya katika masoko ya kimataifa ya kilimo.

**2.24 Mazingatio katika sekta hii yamebadilika kuwa kwenye mgawo wa matumizi ya maendeleo.** Mgawo wa bajeti ya maendeleo uliopitishwa umeongezeka zaidi ya mara dufu kwa asilimia 102.8 katika muda wa mwaka mmoja kutoka shilingi bilioni 13.6 hadi shilingi biliioni 27.6 katika miaka ya afedha 2009/10 na 2010/11 kwa mtiririko huo kama inavyoonekana katika Kielelezo 20.


**2.25 Ongezeko la juu lilitokana na matokeo ya programu ya kuchochea uchumi (Economic Stimulus Programme) iliyokuwa ikitekelezwa katika baadhi ya sekta ndogo za kilimio.** Licha ya mgawo kuongezeka katika kitengo cha maendeleo, kiwango cha kutumika bado kilikuwa chini nakile cha matumizi ya kawaida kikiwa na wastani wa asilimia 74 ikilinganishwa na asilimia 96.1 katika kitengo (vote) cha kawaida. Matumizi kidogo ya

fedha yalishuhudiwa katika mwaka 2010/11 wakati ambapo asilimia 68.7 tu ya fedha ilitumika. Hii ilitokana na matumizi madogo ya fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya programu ya kuchochea uchumi.

## Sekta ya Hifadhi ya Jamii

2.26 **Bajeti ya kawaida iliongoza katika matumizi yaserikali katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.** Tangu mwaka 2009/10, mgawo wa serikali kwa sekta kwa kiasi kikubwa umeongezeka kutoka shilingi bilioni 32.7 hadi shilingi bilioni 371 katika mwaka wa fedha 2011/2012, ongezeko la asilimia 13.5. Kuongezeka kwa mgawo huo kulitokana na matumizi ya juu katika usalama wa chakula katika taifa, maafa na mipango ya hifadhi ya jamii. Hata hivyo, kama asilimia ya jumla ya bajeti ya serikali, matumizi kwa sekta hii yalipungua kutoka asilimia 4.2 mwaka 2009/10 hadi asilimia 3.8 mwaka 2011/12; angalia Kielelezo 21. Matumizi ya bajeti ya kawaida ni zaidi ya asilimia 3 ya bajeti ya serikali na yale ya bajeti ya maendeleo ni chini ya asilimia 0.5.

**Kielelezo 23: Utekelezaji wa bajeti umeboreka....lakini kuna tofauti ya asilimia 20 katikati ya bajeti ya kwaida na ya maendeleo**





*Chanzo: Makadirio ya wafanyikakazi yakitumia akaunti za matumizi ya KENAO na makadirio ya serikali yaliyochapishwa *Ukubwa wa kiputo = Kiasi cha utekelezaji*

2.27 **Sekta iameanzisha sera ya kuendeleza miundo ya kuimarisha uwezo wa nchi ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa manufaa ya walio maskini na walio katika mazingira magumu.** La muhimu kati ya programu zikiwepo kuanzishwa kwa fedha zilizoimarishwa kulinda wanaoishi katika mazingira magumu kutokana na maisha magumu. Katika programu ya kuhamili fedha kwa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, serikali iliongeza mpango na hutoa shilingi 4,000 kila baada ya miezi miwili kama fedha zilizo hamilishwa kwa nyumba zinazofadhili OVCs katika majimbo yote 47. Kufikia Juni mwaka 2012, nyumba 144,933 zilikuwa zinasaidiwa na serikali pamoja na wafadhili, ikilinganishwa na lengo la nyumba 120,000 katika Mpango wa Kwanza wa Kipindi Wastanicha Ruwaza 2030. Programu ya kuhamili fedha kwa wazee (OP-CTP) hutoa shilingi 2,000 kwa mwezi kwa


watu 36,304 waliolengwa katika kaunti 47 dhidi ya lengo la Mpango wa Kwanza wa Kipindi Wastani cha Ruwaza 2030 (MTPI) lililokuwa 33,000. Kielelezo 22 kinaonyesha mwenendo wa ulipaji kwa walengwa wa OP-CTP kwenyekaunti katika kipindi hicho.

**Kielelezo 24: Tofauti zilizofichika za utekelezaji wa bajeti za sekta, 2005-2010**




*Chanzo: Makadirio ya wafanyikakazi yakitumia akaunti za matumizi ya KENAO na makadirio ya serikali yaliyochapishwa *Ukubwa wa kiputo=Kiasi cha utekelezaji*

**Kielelezo 25: Utekelezaji wa sekta ya miundo misingi**





*Chanzo: Hesabu zilizofanywa na wafanyikazi kutumia ripoti ya sekta ya EI&ICT*

**2.28 Kuna fokasi kwenye maendeleo ya biashara kama mkakati muhimu wakuongeza fursa za kiuchumi kwa wanawake na vijana na watu wanaoishi katika mazingira magumu.** Hazina ya biashara ya vijana ilianzishwa kwenye sekta hii ili kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na kutoa huduma za maendeleo ya biashara. Juhudi zimefanywa ili kuwezesha uhusiano katika mitungo ya ugavi, kujenga fursa za soko za bidhaa, ndani na nje ya nchi, na huduma za biasharaza vijana. Kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2011/2012, serikali ilikuwa imetenga shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya hazina hii. Vilevile, hazina ya fedha ya biashara kwa wanawake (Women Enterprise Fund—WEF) iliundwa na serikali katika mwezi wa Agosti, 2007, ikilenga kukuza uwezeshaji wa kiuchumi wa wanawake. Hii ni kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji na utoaji wa mikopo nafuu kwa wanawake kuanza/au kupanua biashara zao kwa ajili ya utajiri na ajira. Mgawo wa fedha kwa hazina hizi mbili umekuwa ukipungua lakini kutokana na mpango wake wakuzunguka kumekuwepo na mafanikio mengi.


**2.29 Uwezo wanyumba kupata huduma za kimsingi zikiwepo elimu, makazi, afya na mavazi umeongezeka.** Katika uwezeshaji wa kiuchumi,inaeleweka kwamba kuna fedha zinazozunguka katika uchumi wa ndani ya nchi. Utamaduni wa kuweka akiba umeanzishwa na umewezesha watu kujihusisha katika biashara ndogo ndogo. Ubora wa maisha ya walengwa pia umeinuliwa. Ongezeko katika kupatikana kwa chakula, upatikanaji wa huduma za afya na upatikanaji wa elimu, ni ishara tosha kwamba kumekuwa na ongezeko kwa mtaji wa kijamii. Juhudi za serikali zinazoendelea za kusaidia vijana kwa njia ya utoaji wa msaada kupitia hazina ya vijana hazijaunda tu nafasi nyingi za ajira kwa vijana, bali pia zimeimarisha utamaduni wa ujasiriamali. Hata hivyo, mahitaji ya dhamana na taasisi ndogo ndogo za fedha ni changamoto kwa upatikanaji wa mikopo kwa vijana.

**Kielelezo 26: Kiwango cha ufyonzaji wa fedha zilizotengwa katika bajeti katika sekta yaafya**




*Chanzo: Makadirio yaliyochapishwa na akaunti za matumizi ya bajeti (KENAO)*

**Kielelezo 27: Ulinganishi wa mapato na matumizi**




*Chanzo: Kauli ya sera ya bajeti, Aprili 2013*


## Utekelezaji wa bajeti umepiga hatua japo maendeleo bado

**2.30 Utekelezaji wa bajeti umeongezeka katika miaka ya hivi punde, hasa katika matumizi ya bajeti ya maendeleo, ingawa bado yapo nyuma.** Utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida umebakia katika kufuatilia kwa kiwango cha utekelezaji wa asilimia 95, lakini kuongezeka katika miaka ya hivi karibuni mpaka asilimia 98 katika mwaka wa 2009 wakati wa mpango wa kichecheo wa

fedha. Kielelezo 23 unaonyesha viwango vya utekelezaji kwa ajili ya bajeti ya kawaida na maendeleo kulinganisha wastani kwa vipindi viwili 2002-2006 na 2007-2010.


**2.31 Utekelezaji wa bajeti ya maendeleo pia umeboreshwa.** Kutoka kiwango cha chini cha asilimia 55 katika mwaka wa 2005, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo umeongezeka mpaka asilimia 75. Ongezeko hili la ajabu linaweza kuhusishwa na mabadiliko katika muundo

**Kielelezo 28: Kwa wastani asilimia 47 pekee ya mikopo ya nje na misaada hutolewa, hii hudhoofisha utekelezaji wa bajeti ya maendeleo**




*Chanzo: Hazina ya Kitaifa, 2013*

**Kielelezo 29: Udhaifu katika mifumo ya usimamizi ya fedha za umma**




*Chanzo: Makadirio ya wafanyikazi*

wa vyombo vya fedha, ambayo imeshuhudia madeni ya kukopa fedha ndani ya nchi yakichukua sehemu kubwa ya bajeti na kupungua kwa umuhimu wa mikopo ya njeya nchi katika bajeti. Utoaji wa mikopo ya njena misaada ni kati ya asilimia 40 na 50 (Tazama Sehemu 1.1 kwa maelezo zaidi).


| Sanduku 1: Ajenda ya mfumo wa ununuzi wa umma, Kenya |
|---|
| Katika kuweka ajenda ya mageuzi ya ununuzi wa umma mbele, serikali ilishiriki katika methodolojia ya OECD / DAC ya kutathmini mifumo ya ununuzi wa umma. Methodolojia hii ina nguzo nne kuu, viashiria 12 na viashiria vidogo 54. Nguzo hizi ni: (i) mfumo wa kisheria na udhibiti, (ii) mfumo wa kitaasisi na uwezo wa usimamizi, (iii) shughuli za ununuzi na mazoea ya soko, na (iv) uadilifu na uwazi wa mfumo wa ununuzi wa umma. Kwa ujumla, mfumo wa ununuzi wa umma wa taifa la Kenya umekuwa na mafanikio ya alama ya jumla ya asilimia 66 juu ya kizingiti cha chini. Kuanzishwa kwa mfumo wa kisheria na udhibiti wa ununuzi, uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi ya Ununuzi wa Umma (PPOA), maendeleo ya mfumo wa utendakazi wa mkataba, na utaratibu mpya wa rufaa, yalikuwa nyanja zilizokuwa na matokeo mema. Nyanja zilizokuwa na matokea duni ni kama uwezo wa kitaasisi katika kununua vyombo na watoa mafunzo, na utendajikazi wa soko la ununuzi. |

**2.32 Hata hivyo, viwango vya utekelezaji vya kijumla vinaficha tofauti za kisekta.** Kulinganisha viwango vya utekelezaji kwa sekta na mfumo wa matumizi ya kipindi cha kati (MTEF) kunaonyesha kwamba utekelezaji ni wa viwango vya juu zaidi katika sekta ya maendeleo ya rasilimali za kibinadamu. Elimui na viwango vya juu zaidi katika utekelezaji wa bajeti (Kielelezo 24). Utekelezaji wa bajeti katika sekta za miundo misingi bado hazijafika kizingiti cha asilimia 80 ila katika mwaka wa 2009 uliohusishwa na programu ya kuchochea uchumi.

**2.33 Utekelezaji wa bajeti katika sekta ya miundo misingiumekuwa wa wastani wa asilimia 77 katika muongo uliopita.** Hata hivyo, kumekuwa na kumbukumbu ya kuboreka kunakoendelea katika miaka ya hivipunde. Ujumlawa ufyonzaji wa fedha zilizotengwa uliongezeka kutoka asilimia 81 mwaka 2009/10 hadi asilimia 84 mwaka 2011/12 (Kielelezo 25). Utekelezaji wa bajeti ya maendeleo umekuwa wa kiwango cha wastani cha asilimia 77 katika kipindi hiki. Changamoto za utekelezaji wa bajeti kwa ajili ya miundo misingi si mpya. Sekta inachukua sehemu kubwa ya rasilimali za nje ambazo zina viwango vya chini vya utoaji (kama inavyoonekana katika Sehemu 1.1); sekta pia ina miradi mikubwa na mahitaji ya masharti magumu ya ununuzi ambayo huchelewesha utekelezaji.

**2.34 Fauka ya hayo, viwango vya chini vya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo vinadhoofisha matumizi kwa ajili ya mitambo/majengo katika sekta ya afya.** Kielelezo 26 kinaonyesha kwamba katika utekelezaji wa bajeti katika sekta ya afya, matumizi ya kawaida ni zaidi

**Kielelezo 30: Maendeleo ya deni la taifa la Kenya**





*Chanzo: Makadiriio ya wafanyikazi kutumia data kutoka wizara ya wizara ya hazina ya taifa na Shirika la Fedha Duniani (IMF)*

kwa asilimia 80 lakini matumizi ya maendeleo yako nyuma na asilimia 65. Hivyo, matumizi ya mitambo/majengo katika sekta yanakuwa chini ya asilimia 10 ya bajeti.

Kuboreshwa kwa jumla katika utekelezaji wa bajeti kunaweza kuhusishwa na uwezo wa kutafuta rasilimali za ndani kufadhili bajeti kwa kuchunguza mapato na mikopo ya ndani, na kwa kiasi cha mageuzi ya ununuzi ya hivi karibuni.

**2.35 Tofauti katika viwango vya utekelezaji kati ya matumizi ya mitambo/majengona bajeti ya rasilimali zinazotumika inahusishwanavyanzovyafedha.** Malipo ya kwanza juu ya mapato yanayopatikana nimalipo ya riba, ujira na mishahara, na pensheni, ikifuatiwa na matumizi ya shughuli/ utendaji. Matumizi ya maendeleo yanafadhiliwa pakubwa kupitia madeni ya ndani na mikopo ya nje na misaada. Kielelezo 27 kinaonyesha vyanzo vya

**Kielelezo 31: Mtungo wa madeni ya ndani umebadilika**





*Chanzo: Makadirio ya wafanyikazi kutumia data ya Benki Kuu ya Kenya*

fedha upande wa kushoto na matumizi upande wa kulia, vikipangwa kwa kipaumbele kutoka juu chini. Kielezo kinaonyesha kwamba utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida unategemea mapato wakati utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya maendeleo unategemea uwezo wa kufikia malengo ya mikopo ya ndani kwa upande mmoja na utoaji wa mikopo ya nje na misaada kwa upande mwingine.

**2.36 Utekelezaji wa bajeti huiga viwango vya pesa zinazopokelewa na hazina ya taifa.** Kielelezo 28 kinaonyesha pesa zilizopokelewa nahazina ya taifa kama sehemu ya makadirio ya bajeti kwa miaka mitatu kutoka 2011 hadi Machi 2013 (robo tatu ya mwaka wa fedha). Katika miaka hii mitatu, asilimia 86 ya mapato ya bajeti ilikusanywa, asilimia 74 ya madeni ya ndani iliyopangwa ilitolewa na asilimia 47 ya bajeti ya mikopo kutoka nje na misaada ilikuwa imetolewa. Kutopokea kwa hazina ya taifa pesa ilizotarajia ni mojawapo ya sababu ya viwango vya chini vya utekelezaji wa bajeti na kutolipia matumizi yanaongeza hisa ya malimbikizo ambayo hayajalipiwa.

**Kielelezo 32: Utendaji wa mapato na matumizi ya Kenya ikilinganishwa na nchi zingine**





*Chanzo: Benki ya dunia, viashiria vya maendeleo ya dunia, 2012*

**2.37 Sheria ya usimamizi wafedha za umma ya 2012 ina lengo la kushughulikia changamoto zilizokoza usimamizi wa fedha za umma na kufanya upya mifumo ya usimamizi, hivyo kuboresha ufyonzaji wa pesa zilizotengwa katikabajeti.** Hata hivyo, tahadhari kubwa inatakikanaili kuwezesha utekelezaji ulio sahihi katika wizara husika na hasa katika serikali za kaunti. Kielelezo 29 kinatoa muhtasari wa baadhi ya udhaifu katika mifumo wa usimamaizi wa fedha za ummaunaoathiri ufanisi wa matumizi ya umma nchini Kenya.

**2.38 Kukubali mageuzi pia kutatoa matumaini kwa ajili ya utekelezaji bora wa bajeti.** Utekelezaji mdogo wa bajeti mara nyingi umehusishwa nakutofanya vizuri kwa mifumo ya ununuzi. Miradi ya maendeleo nimizito na inahitaji zabuni ya ushindani ambayo inaweza kuwa ndefu na wakati mwingine kupingwa na wagombea walioshindwa ambao kwa hasira huchelewesha utekelezaji. Mabadiliko ya hivi karibuni katika utekelezaji yanaweza


kuhusishwa na mabadiliko yanayoendelea katika mifumo ya ununuzi (angalia Sanduku 1). Mifumo ya kina ya sheria, kanuni na taasisi za usimamizi imetengenezwa kusimamia na kudhibiti taratibu za ununuzi wa serikali na kazi. Mfumo wa kisheria kwa jumla unachukuliwa kuwa kamili/timamu na ni mazoea mazuri kwamba nyaraka za zabuni zitengenezwe. Hata hivyo, uwezo wa utekelezaji unakwamishwa kutokana na kutokuwa na wafanyikazi wa kutosha pamoja na ufadhili mdogo wa shughuli za ununuzi katika wizara husika.

**Kielelezo 33: Upungufu katika mapato yameendelea tangu 2008/09**




*Chanzo: Shirika la Ushuru la Kenya*

**Kielelezo 34: Mchango kwa jumla ya mapato ya kodi**




*Chanzo: Shirika la Ushuru la Kenya*

## Madeni yameongezeka lakini bado yako ndani ya mipaka inayokubalika


**2.39 Madeni ya umma yameongezeka lakini bado yako ndani ya mipaka inayokubalika, karibu asilimia 44 ya Pato la Taifa.** Mageuzi ya madeni ya umma yanaweza kuonekana kupitia nakisi ya msingi; mfumo wa fedha ulioweka kumbukumbu ya baki la msingi kati ya mwaka 2003 na 2005 na bajeti ya uwiano kati ya mwaka 2006 na 2007, na kipindi cha uimarishaji wa fedha. Upunguzaji wafanyikazi wa serikali uligeuka kuwa kichocheo na nakisi ya msingi wa wastani wa asilimia 2.5 kati ya mwaka 2008 na 2011. Harakati hizi katika nakisi ya msingi zinajitokeza katika kuongezeka kwasehemu ya madeni kutoka asilimia 39 katika mwaka 2007 hadi asilimia 47 mwaka 2012 (angalia Kielelezo 30).

**2.40 Nafasi ya kifedha iliundwa kupitia uimarishaji wa programu ya kuchochea uchumi ya miaka 2009 na 2011.** Serikali ilitoa madeni zaidi ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuondoa hatari ya mtikisiko wa kiuchumi. Hivyo, deni kama sehemu ya Pato la Taifa imeongezeka kwa karibu pointi asilimia 5 kutoka asilimia 39 katika mwaka 2007 hadi asilimia 44 mwishoni mwa 2012 lakini bado ipo chini ya lengo la sera ya asilimia 45. Katika tathmini asili madeni ya umma yameongezeka kutoka shilingi bilioni 700 mwaka 2007 hadi shilingi trilioni 1.4 mwishoni mwa 2012. Kielelezo 27 kinaonyesha jumla ya madeni hisa ikigawanywa kati ya madeni ya ndani na nje (shilingi bilioni), na deni kama sehemu ya Pato la Taifa.

**2.41 Vyombo vya madeni ya ndani sasa vyaruhusu uwekezaji wa muda mrefu.** Mwanzoni mwa muongo (2002) bili za hazina zilifadhili asilimiai 49 ya upungufu/ nakisiwa bajeti; leo sehemu hii imepungua kwa asilimia 19 (Kielelezo 31). Mwenendo huu unaonyesha mafanikio ya lengo la sera ya uwiano 25:75 ya bili za hazina nahati za ukopeshaji. Hivyo, kupitia utoaji wahati za ukopeshaji, serikali inaweza sasa kufadhili miradi ya maendeleo kwa muda mrefu bila ya utegemezi mkubwa wa fedha za nje. Uwezo wa kuhamasisha rasilimali za ndani ya nchi umeshuhudia kupungua kitaratibu kwa umuhimu wa fedha za nje katika bajeti (Hii imejadiliwa katika Sehemu 1.1.

**2.42 Mienendo ya madeni yanaonyesha maendeleo matatu muhimu ya fedha ambayo yana thamani kuangaziwa.** Kwanza, yanaonyesha ahadi ya kugharamia programu za maendeleo ya miundo misingi kamailivyoainishwa katika Ruwaza ya 2030, kuunganisha bajeti na mipango. Pili, inaonyesha uwezo wa kutafuta rasilimali za ndani na nje ambao awali ulikuwa ukizuia utekelezaji wa bajeti. Tatu, huonyesha uwezo wa mfumo wa fedha kudhibiti majanga ya kiuchumi kupitia upunguzaji wa fedha na upanuzi kama inavyofaa. Historia ya usimamizi wa madeni ya Kenya unapata B+ katika mikopo iliyotoka kiwango cha "kawaida na duni" na haijawahi kuwa katika kitengo cha "nchi zenye madeni makubwa".

**Kielelezo 35: Ongezeko katika matumizi ya umma yalileta kuimarika kwa ukuaji wa Pato la Taifa katika mwaka wa 2009-2011**




*Chanzo: Makadirio ya wafanyakazi kutumia datakutoka KNBS*

### Mfumo wa fedha una uwezo mkubwa lakini Kodi ya Nyongeza ya Thamani haitendi kazi vyema

2.43 **Mapato kama sehemu ya Pato la Taifa yako na wastani wa karibu asilimia 22 ambayo ni mojawapo ya zile zilipo juu kabisa katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara na kwa uhakika ni ya juu zaidi katika jumuiya ya Afrika mashariki (EAC).** Uwezo wa mapato ya Kenya unalingana vizuri na majirani kama Uganda, Tanzania na Ethiopia. Kielelezo 32 kinaonyesha mapato na matumizi ya nchi za Kiafrika zilizochaguliwa; kielelzo kinalinganisha wastani katika vipindi viwili, Kenya na Afrika Kusini zipo mbele ya nchi zingine. Hata hivyo, uchambuzi wa utendaji wa kodi mbalimbali unaonyesha kwamba ni kodi ya mapato tu ndio inaendeleza ukubwa wa mfumo wa kodi ya Kenya wakati kodi nyingine hazifanyi vyema ikilinganishwa na malengo yaliyokusudiwa, hasa Kodi ya Nyongeza ya Mapato.

2.44 **Ni kodi ya mapato pekee inayoaendeleza mfumo wa kodi, ikichangia zaidi ya asilimia 40 ya jumla ya mapato.** Kielelezo 33 kinaonyesha tofauti kati ya malengo ya mapato na makusanyo halisi. Tangu 2009, ukusanyaji wa mapato umepunguachini ya malengo. Kodi ya mapato tu ndiyo iliyoimarika katika ukuaji wa mapato. Jumla ya mapato yameongezeka pakubwa kati ya miaka 2004 na 2011, kutoka shilingi milioni 207,563 mwaka 2004 hadi shilingi milioni 669,442 mwaka 2011. Hii imekuwa inaongozwa na kodi ya mapato ambayo iliongezeka kutoka asilimia 6 ya Pato la Taifa mwaka 2001 hadi asilimia 10 mwaka 2012, na sasa ni asilimia 40 ya jumla ya mapato. Utendaji bora wa kodi ya mapato kwa kiasi kikubwa umehusishwa na ulipaji wa kodi zaidi baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa kutathmini kodi ya kibinafsi na matumizi ya nambari binafsi ya utambulisho (PIN) kwa madhumuni ya tathmini ya kodi. Kielelezo 33 kinaonyesha mchango wa mapato kama asilimia ya Pato la Taifa wakati makusanyo ya kina ya mapato na malengo yanapatikana katika Kiambatanisho cha 3.

2.45 **Sehemu ya Kodi ya Nyongeza ya Thamani imepungua kutoka asilimia 18 ya mapato ya jumla mwaka 2004 hadi asilimia 15.4 mwaka 2011.** Kukusanya kodi ndogo kunasababishwa na maswala ya nje na ya ndani. Kutolipa kodi, hasa matumizi ya mitambo ya elektroniki ya kodi (ETR), nisababu kubwa ya kupungua kwa kodi hiyo. Baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa ETR, kiwango cha uzingatiaji waasilimia 90 ulilengwa (KRA, 2012). Hata hivyo, utafiti wamwaka 2009/10 uligundua kuwa wakati uwekaji mitambo ulikuwa juu kwa asilimia 98, matumizi (kufuata) yalikuwa katika kiwango kati yaasilimia 60-65. Sababu ya pili na pengine iliyo ya muhimu zaidi inayoelezea nakisi ya mapato ni kushuka kwa matumizi katika miaka michache iliyopita (Kielelezo 34), ambayo kwa upande ina madhara makubwa kwa kodi zisizokuwa za moja kwa moja kulinganishwa na kodi za moja kwa moja.

2.46 **Kwa ujumla, sehemu ya ongezeko la kodi ya mapato katika jumla ya mapato ya kodi na kupungua kwa Kodi ya Nyongeza ya Mapato si sambamba na sera ya serikali iliyokusudiwa kubadilisha kutegemea kodi za moja kwa moja kuelekea kodi zisizokuwa za moja kwa moja.** Mabadiliko ya sera kutokakwa kodi za moja kwa moja hadi zile zisizokuwa za moja kwa mojayalilenga kupunguza mzigo wa kodi ya mapato ili kuchochea akiba na uwekezaji. Ukuaji wa polepole hasa wa Kodi ya Nyongeza ya Thamani (VAT) na mapato ya ushuru ya bidhaa yametokana na sababu mbili: kiwango kidogo cha kulipa kodi, na ukweli kwamba sheria ya sasa ya Kodi ya Nyongeza ya Thamani haitozwi kwa bidhaa kadha wa kadha.

2.47 **Uchambuzi wetu unaonyesha kwamba mfumo wa kodi wa Kenya ni imara;** ukuaji wa asilimia 1 ya Pato la Taifa lazima ushuhudie ongezeko la asilimia 1.26 ya mapato katika muda mrefu. Ukadiriaji wa kisayansi wa uhusiano kati ya ukuaji wa Pato la Taifa na ukuaji katika kodi (ukiondoa hatua mpya ya kodi ya hiari katika kila bajeti) inaonyesha kwamba ukuaji katika mapato ya kodi lazima yapite ukuaji katika Pato la Taifa: ukuaji wa asilimia 1 katika Pato la Taifa lazima lishuhudie ukuaji wa asilimia 1.26 kwa mapato. Hata hivyo, uchambuzi unaonyesha kwamba ni ukuaji katika kodi ya mapato tu ndio unapita ukuaji katika msingi wake. Ukuaji katika mapato ya ushuru na Kodi ya Nyongeza ya Thamaniupo chiniya viwango vya ukuaji wa misingi yao ambayo ni matumizi (Kiambatisho 4 kinalinganisha ukuaji katika kila aina ya mapato na misingi yake).

### Mfumo wa fedha unaweza kustahimili misukosuko ya kiuchumi

2.48 **Usimamizi wa fedha wenye busara umesaidia uchumi wa Kenya kustahimili misukosuko na athari za kindani.** Kuongezeka kwa matumizi ya umma mwaka 2009-2011 kuliimarisha mahitaji hivyo kuzuia msukosuko wa uchumi. Nafasi ya fedha iliyoundwa na viwango vya chini vya madeni iliruhusu programu ya kuchochea uchumi ya 2009-2011, ambayo iliongeza matumizi ya serikali kwa asilimia 30 ya Pato la Taifa na kuhimiza mahitaji katika uchumi wa ndani. Kwa hiyo, uchumi uliweka kumbukumbu ya ukuaji wa wastani wa asilimia 3.6. Wakati wa kipindi cha kuchochea uchumi,matumizi ya serikali yalichangia asilimia 1 hadi asilimia 3.9 ya ukuaji wa Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 0.4 wakati wa kuimarisha fedha. Wakati huu, ukuaji wa Pato la Taifa lilikuwa kwa watani wa asilimia 5.4. Mchango kwa ukuaji kutoka sehemu nyingine za mahitaji (matumizi binafsi, uwekezaji na mauzo ya nje) ulipungua kutoka asilimia 5 hadi asilimia 2.6 kati ya vipindi hivi viwili. Kielelezo 35 kinalinganisha ukuaji wa wastani katika vipindi viwili, uimarishaji wa fedha (2003-2007) na vipindi vya kuchocheo uchumi (2008-2011).


2.49 **Programu ya fedha sasaipo nyuma ya uimarishaji lakini mabano ya matumizi ya muda/ kipindi cha kati yanafifisha matarajio ya mafanikio.** Kupunguzwa kwa matumizi ya umma kulisaidia kurejesha utulivu katika mwaka 2011. Nchi ilishuhudia kipindi cha udhaifu wa uchumi katika mwaka wa 2011, nakisi ya akaunti ya hundi iliongezeka na gharama ya bidhaa kutoka nje ya nchi iliongezeka zaidi pamoja nakudhoofika kwa shilingi dhidi ya sarafu zote kuu za dunia. Katika kukabiliana na mgogoro huo, matumizi ya umma yalikuwa yamepunguzwa ili kukabiliana na mahitaji ya uagizaji wa bidhaa. Mfumo wa kipindi cha wastani cha fedha unaonyesha kushuka kwa taratibu katika jumla ya nafasi ya fedha kama sehemu ya Pato la Taifa lakini kukiwa na shinikizo kubwa la matumizi.

Sura ya 3

# MAKADIRIO YA WAKATI WA WASTANI: MFUMO WA FEDHA WASUKWASUKWA

3.1 **Mwaka wa Hazina wa 2013 unaadhimisha mwanzo wa ugatuzi ambao unaenda sambamba na serikali mpya—ambayo inajaribu kutimiza ahadi zake za kabla ya uchaguzi.** Shinikizo za matumizi ya fedha zitaongezeka katika muda wa wastani wakati ambapo serikali za kaunti zinapoanza kufanya kazi huku serikali mpya ikitafuta mbinu za kutimiza ahadi za kabla ya uchaguzi. Shinikizo hizi zitazidishwa na ongezeko la mishahara ya wafanyikazi wa umma wakati ambapo mapato ya serikali yamekuwa hayatoshi kwa muda mrefu. Katika mwaka wa bajeti wa 2012/13, nyongeza ya mishahara ya wafanyikazi wa umma ilifikia karibu Shilingi bilioni 30 (asilimia 1 ya Jumla ya Pato la Serikali). Katika sehemu hii, tutagusia makadirio katika muda wa wastani na shinikizo za kifedha zinazochipuka.

**Kielelezo 36: Njia ya ugavi wa mapato unatenga asilimia 23 ya mapato ya serikali kwa ajili ya serikali za kaunti**




*Chanzo: Kutoka kwa Hazina ya Bajeti ya Kitaifa 2013/14, Juni 2013*


## Maendeleo ya kifedha ya hivi punde

3.2 **Mwanzo wa ugatuzi: Serikali za kaunti zimeanza na bajeti ya kwanza kamili baada ya Katiba ya mwaka wa 2010 imewasilishwa Bungeni.** Mfumo wa kifedha wa

muda wa wastani umechukua mwelekeo wa ugavi wa mapato katika njia ya wima kati ya serikali kuu na serikali za kaunti, na ugavi mfuo kati ya serikali za kaunti. Bajeti ya kwanza imetenga asilimia 32 ya mapato kwa ajili ya serikali za kaunti. Hii ni sawa na asilimia 34.5 ya mapato yaliyo kaguliwa.[1] Hata hivyo, ijapokuwa mgawo wa fedha kwa serikali za kaunti iko juu ya kadiri iliyo ndogo inayopendekezwa na Katiba, magavana wa kaunti wanasema kwamba mgawo huo ni mdogo na hauwezi kuleta mabadiliko yoyote ya kimaendeleo ama kuboresha huduma katika. Kwa hivyo, serikali za kaunti zitaendelea kuwa chanzo cha shinikizo za kifedha. Kwa ujumla, ongezeko la matumizi ya kawaida lazewa kudhoofisha kufikilia malengo ya matumizi.

**3.3** **Hata hivyo, mapendekezo ya kifedha katika wakati wa wastani na sera za serikali zinaonyesha kuendelea kwa nidhamu ya kifedha.** Mapato yanakadiriwa kufikia asilimia 24 ya Mapato ya Serikali huku makadirio ya matumizi yakionekana kushuka kutoka asilimia 32 ya Mapato ya Serikali katika mwaka wa 2013 hadi asilimia 30 katika mwaka wa 2014 na asilimia 29.5 katika mwaka wa 2015. Kuimarika huku kutashukisha upungufu wa bajeti kutoka asilimia 6.8 katika mwaka wa 2013 hadi asilimia 4.0 katika mwaka wa 2015 na upungufu wa deni ikilinganishwa na Mapato ya Serikali kutoka asilimia 45.6 hadi 44.2 katika muda wa wastani. Mfumo wa kifedha katika muda wa wastani umeoneshwa katika Kiambatisho 1. Hata hivyo, tukitilia maanani chipuko la shinikizo za kifedha, nidhamu zaidi ya kimatumizi ya fedha itahitajika ili kugharamia deni na kufikilia malengo ya upungufu wa bajeti yanayozingatiwa.

**Kielelezo 37: Mapato ya kodi ya nyongeza ya thamani yataongezeka iwapo bidhaa zote zitatozwa kodi**





*Chanzo: Uigizaji wa Wafanyikazi ukitegemea data ya Shirika la Kutoza Ushuru la Kenya (KRA)*

## Upungufu wa mapato utashinikiza mahitaji ya kifedha Revenue

[1] *Katiba imetenga asilimia 15 ya mapato yaliyokaguliwa ya mwaka wa awali kama kiasi kidogo kinachokubalika kama mgawo sawa kwa ajili ya serikali za kaunti na asilimia 0.5kama hazima ya kusawazisha maendeleo katika kaunti zenye umasikini mkubwa. Mapato yanayohitajika kugawanywa ni mapato ya kawaida na hayazingatii faini na ushuru unaokusanywa na wizara mbalimbali. Mapato yaliyokaguliwa ni ya mwaka wa 2010/11 ambapo mapato yanayohitajika kugawanywa ni Shilingi bilioni 608.*

**3.4 Ukusanyaji wa mapato katika miaka ya hivi punde (tangu 2009) umeshindwa kufikilia malengo ya bajeti.** Kwa mfano katika mwaka wa 2012/13, upungufu wa bajeti miezi tisa kabla ya mwaka wa bajeti ulikuwa Shilingi bilioni 82 (kama US$ 1 bilioni). Kuzingatia hatari hii, hazina ya kitaifa ya fedha imeamua kulinda bajeti za kaunti kutokana na upungufu wa mapato.

**Kielelezo 38: Madai ya mshahara wa wafanyikazi wa Kenya yakilinganishwa na nchi nyingine za Afrika (Kama asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali)**




*Chanzo: Shirika la Fedha Duniani (IMF) 2013*


**3.5 Mswada wa Kodi ya Nyongeza ya Thamani (VAT) unaongojea uamuzi wa Bunge utashughulikia changamoto hizi kwa kuongeza njia za kupata ushuru wa serikali.** Mswada wa Kodi ya Nyongeza ya Thamani 2012 ulipitishwa Bungeni mwaka huu. Mswada huo unapendekeza kuongeza ushuru kwa kupunguza bidhaa zilizokuwa hazitozwi kodi ya nyongeza ya thamani. Uanzilishi wa ushuru wa mauzo kwa biashara ndogo zenye mauzo chini ya shilingi milioni 5 utaongeza ushuru wa serikali. Hata hivyo, jitahada kubwa bado inahitajika katika usimamizi wa shughuli za kutoza ushuru na kupunguza kukwepa kulipa ushuru. Kielelezo 37 unaashiria vile ambavyo kodi ya nyongeza ya thamani inavyoweza kukusanywa iwapo bidhaa zote ambazo hazitozwi ushuru huu zitaanza kutozwa. Kielelezo pia unaonesha uwezekano wa jumla ya kodi ya nyongeza ya thamani wakati imekarabatiwa hadi asilimia 60 ya ubora wa usimamizi. Hata hivyo, mswada wa kodi ya nyongeza ya thamani 2012 ulipendekeza kutotozwa ushuru huo kwa bidhaa na huduma. Orodha kamili inaonesha mapendekezo ya kodi ya nyongeza ya thamani imepeanwa katika Kiambatisho 5. Kwa ujumla, Kielelezo unaonesha kuna nafasi ya kuongeza ukusanyaji wa kodi ya nyongeza ya thamani.

## Ongezeko la mishahara ya wafanyikazi wa umma likaathiri vibaya mfumo wa kifedha

**3.6 Madai ya fedha ya mishahara ya wafanyikazi wa umma wa Kenya yako juu ikilinganishwa na ile ya viwango vya kimataifa.** Ikiwa kati asilimia 7.9 ya Jumla ya Mapato ya Serikali katika mwaka wa 2012, madai ya fedha ya mishahara ya wafanyikazi wa umma wa Kenya yalikuwa juu ikilinganishwa na mataifa mengine katika Afrika Mashariki. Hata hivyo, ilikuwa chini kidogo ikilinganishwa na uchumi wa nchi zingine za Afrika zilizo na uchumi bora hasa Afrika Kusini, Botswana na Angola (Kielelezo 38).


3.7 **Katika muongo uliopita, Kenya imeshuhudia kupungua kwa madai ya mishahara ya katika sekta ya umma.** Hata hivyo, mwelekeo huu umeanza kubadilika: madai ya mishahara ya wafanyikazi wa umma yameanza kuongezeka na ugatuzi wa serikali utazidisha shinikizo za kifedha. Katika mwaka wa 2012, wafanyikazi mbalimbali wa umma walianza kudai nyongeza ya mishahara. Walimu, ambao wanajumulisha asilimia 50 ya mishahara ya wafanyikazi wa sekta ya umma, waliandamana na mwishowe kudai nyongeza ya mshahara ya asilimia 48.6 kwa mwalimu anayelipwa kiasi cha chini zaidi na nyongeza ya asilimia 18 kwa anayelipwa kiwango cha juu zaidi. Wauguzi, madaktari na wahadhiri pia waliweza kudai nyongeza zao. Katika mwaka wa 2013, jumla ya nyongeza zote zilikuwa ni Shilingi bilioni 30 ama asilimia 1.0 ya Jumla ya Mapato ya Serikali[2]. Isitoshe, mpangilio mpya wa serikali umeleta vitengo vya usimamizi katika viwango vyote vya serikali—Bunge, Ofisi ya Rais na Idara ya Mahakama—utaongeza madai ya mishahara ya wafanyikazi wa umma. Ongezeko hili linaonekana katika mabadiliko ya mpangilio wa madai ya mishahara ya wafanyikazi wa umma yakilinganishwa na Jumla ya Mapato ya Serikali kuanzia mwaka wa 2012 (Kielelezo 39). Tukio sawa lilishuhudiwa mwaka wa 2013.

**Kielelezo 39: Madai ya misharaha yaongezeka**




*Chanzo: Maelezo ya Sera ya Bajeti 2013*

**Kielelezo 40: Serikali za kaunti zitapata Shilingi bilioni 210 ambazo magavana wanalalamika kuwa hazitoshi**




*Chanzo: 2013/14 Maelezo ya bajeti ya hazina ya fedha nchini (Juni 2013)*

*2 Ni muhimu kukumbuka kwamba mishahara ilikuwa haijabadilishwa tangu mwaka wa2008, hata baada ya mfumko wa bei ulipofikia kiwango cha juu na kufikia wastani wa asilimia 14 katika mwaka wa 2011.*

3.8 **Tume ya Mishahara ya Wafanyikazi wa Umma (SRC) imeanzisha upatanishaji wa mishahara ya wafanyikazi wa umma lakini pana hatari kwamba shughuli hii inaweza kukumbwa na siasa.** Tayari, wabunge wamedai kubaki na mishahara yao ya awali baada ya mgogoro wa muda mrefu na Tume ya Mishahara ya Wafanyikazi wa Umma. Walimu pia wamedai nyongeza ya mishahara na wafanyikazi wengine wananung'unika. Tume ya Mishahara ya Wafanyikazi wa Umma yahitaji kulindwa kutokana na siasa na tume iwe na nguvu zaidi kuchukua nafasi inayofaa katika kutoa maagizo kuhusu mishahara na mipangilio ya sekta nzima ya umma.

## Shinikizo kutoka kwa serikali za kaunti

3,9 **Matumizi ya kawaida yanaonekana kuongezeka wakati ambapo serikali za kaunti zinapochukua mamlaka (Kielelezo 40) na hasa kama kutakuweko urejeleaji wa huduma kati ya serikali ya kitaifa na zile za kaunti.** Katika bajeti ya muda wa wastani, gharama ya usimamizi wa ugatuzi unakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 10.5 katika mwaka wa 2013 ikiongezeka hadi Shilingi bilioni 14 katika mwaka wa 2014. Jumla ya pesa hizi inawakilisha malipo ya usimamizi wa kaunti pamoja na bunge la kaunti (Shilingi bilioni 5.9), matumizi ya usimamizi (Shilingi bilioni 1.7), matumizi ya uongozi wa kifedha wa kaunti (Shilingi bilioni 5.6), na bodi za huduma za kaunti za umma (Shilingi bilioni 0.8).

**Sanduku 2: Malengo kadhaa ya kifedha ya muda wa wastani**

Malengo Kadhaa ya Kifedha ya Serikali

**Malengo ya Mapato**
- Ongeza uwiano wa mapato-kwa-Jumla ya Mapato ya Serikali ufikie asilimia 24.5 ifikapo mwaka wa 2015/16.
- Mgawo wa serikali ya kitaifa wa mapato ya kugawanywa upungue hadi chini ya asilimia 30.

**Matumizi**
- Asilimia 30 ya matumizi yatakuwa matumizi ya maendeleo ya kitaifa na pia katika viwango vya kaunti.
- Asilimia 40 ya matumizi ya maendeleo itagharimiwa kupitia mikopo na misaada ya kifedha na misaada mingineyo.
- Asilimia 6.7 ya mapato ya kawaida yatagharimia miradi ya maendeleo iliyopangwa na pia kulipa mikopo.
- Matumizi ya lazima na yanayohitajika kisheria yatakuwa asilimia 17.9 ya malipo ya kawaida yanayotarajiwa.
- Matumizi kwa ajili ya kuendeleza shughuli yatakuwa asilimia 40.4 ya mapato ya kawaida.

**Madai ya mishahara**
- Malipo ya wafanyikazi katika viwango vya kitaifa na serikali za kaunti yatakuwa asilimia 35% ya malipo ya kawaida yanayotarajiwa.

**Upungufu wa fedha na deni la umma**
- Deni la umma likilinganishwa na Jumla ya Mapato ya Serikali liwe chini ya asilimia 45.
- Fikilia uwiano wa 75:25 kwa deni la muda mfupi ikilinganishwa ma deni la muda mrefu.
- Mikopo ya nje ya nchi itagharimu kutokea asilimia 2.5 hadi asilimia 3 ya mapato ya kawaida.

3.10 **Kando na matumizi ya usimamizi, shinikizo la kuongezea serikali za kaunti pesa litaongezeka hasa wakati ambapo serikali hizi zitakapoanza majukumu.** Katiba yasema kuwa fedha zafaa kugawanywa kulingana na majukumu. Kufuatia mwelekeo huu, hazina ya fedha nchini imekadiria matumizi ya kitaifa na majukumu ya ugatuzi kwa kila sekta itakuwa kama ifuatayo kwenye Kielelezo 41.


3.11 **Jukumu moja la ugatuzi ni kudumisha afya bora lakini mgawo wa serikali za kaunti ni kama asili mia 50 hivi ya jumla ya matumizi;** kwa ukulima na miundo misingi, migawo ni asilimia 25 na 27 mtawalia. Migawo hii pengine iko chini sana kuweza kuchangia katika huduma bora, kwa hivyo shinikizo za madai ya mgawo zaidi yanatarajiwa kutoka kwa serikali za kaunti. Isitoshe, ugatuzi umegharamikiwa na bajeti ya serikali ya kitaifa na kuingizwa katika hazina ya ugavi sawa wa serikali za kaunti. Kutengewa fedha hizi hakuna masharti yoyote, kwa hivyo, serikali za kaunti hazina wajibu wowote kuendeleza ugavi wa kisecta mbalimbali kama ilivofanya serikali ya kitaifa hapo awali.

### Shinikizo la kudumisha viwango vya matumizi katika viwango vya sasa ili kuziua ukatizaji wa huduma

3.12 **Katiba inatoa karibu asilimia 15 ya mapato ya kawaida kama mgawo wa sawa kwa serikali za kaunti na pia asili mia 0.5 zaidi ya malipo kwa kaunti zenye umaskini mkubwa.** Tume ya Ugavi wa Mapato (CRA) iliunda utaratibu wa kutenga migawo ya kaunti ikitumia vigezo vitano: idadi ya watu, mgawo wa unaotoshana, kiwango cha umaskini, ukubwa wa ardhi na nidhamu ya kifedha. Punde tu utaratibu huu unapotumiwa, bajeti za kaunti zingine hazitafikia lengo gharama ya sasa ya huduma za ugatuzi. Hii ni sehemu ya agenda ya usawazishaji. Mapato yakigawanywa kila mtu kwa kila kaunti yameoneshwa katika Kielelezo 42. Kielelezo kinaonyesha kuwa kaunti zilizo na watu wengi zina uwezekano wa kutofaidika wakati ambapo utaratibu huu utakpotumika kwa sababu kaunti hizo zitapata mgawo mdogo zaidi kwa kila mtu.

3.13 **Kwa miaka mitatu ya kwanza, Tume ya Ugavi wa Mapato imetambua kaunti 14 ambazo zitanufainika kama kaunti za kwanza katika kupata mgawo wa hazina ya usawazishaji wa maendeleo, zikipokea kati ya Shilingi milioni 271 na Shilingi milioni 186.** Kaunti zinginezo zitalazimika kukidhi mahitaji miradi ya kimsingi kutoka kwa mapato yao na kutoka kwa mgawo kwa kaunti. Kielelezo 42 unaonesha kaunti kulingana na mgawo wa kila mtu katika kaunti kuzingatia usawa wa migawo, miradi ya wafadhili na hospitali za kiwango cha 5 na hazina ya usawazishaji wa maendeleo.

**Kielelezo 41: Mgawo wa kila mtu kwa kaunti 2013/14**




*Chanzo: Mahesabu ya wafanyikazi kulingana na migawo ya bajeti za kaunti (Juni 2013) data*


Sura ya 4

# MATUMIZI YENYE MATOKEA BORA

## Utambuzi kutoka kwa uchunguzi wa vigezo vya ubora wa huduma katika sekta ya elimu ya Kenya

4.1 **Sekta ya elimu hutumia asilimia 30 ya jumla ya makadirio ya matumizi ya kawaida katika bajeti na kama asilimia 70 hivi ya bajeti itatumika katika sekta ya maendeleo ya huduma za kibinadamu.** Sekta hii pia ina viwango vikubwa zaidi vya utendaji: na hili si jambo la kushangaza kwa sababu asilimia 70 ya bajeti ya sekta ya elimu ni mishahara ya walimu na asilimia 20 ni kwa ajili ya mpango wa elimu ya bure na msaada kwa ajili ya elimu ya sekondari ambayo hupeanwa (japo wakati mwingine hucheleweshwa sana) mwishowe. Kielelezo 43 unaonesha migawo ya bajeti na viwango vya utekelezaji wake katika sekta za kijamii—elimu, afya na huduma za kijamii—na kufuatilia maendeleo kwanzia mwaka wa bajeti 2005/06 na utendaji wastani wa muda wa 2006-2010.

**Kielelezo 42: Sekta ya elimu yaongoza katika utekelezaji wa bajeti, 2005-2010**




*Chanzo: Makadirio ya wafanyikazi wa KIPPRA kulingana na makadirio yaliyochapishwa KENAO*

4.2 **Sekta imedumisha zaidi ya asilimia 20 ya fungu la bajeti ya Kenya inayokua.** Zaidi ya

asilimia 90 ya bajeti hii ilitumika kwa malipo na marupurupu ya wafanyikazi katika muda wa 2009/10 to 2012/13 (Jedwali 4). Wakati huohuo, upataji warasilimali zisizo za kifedha ulikuwa katika wastani wa asilimia 3.5. Ongezeko la malipo ya wafanyikazi lilitokana na ongezeko la idadi ya walimu pamoja na ongezeko la wastani wa mshahara. Rasilimali zaidi zilielekezwa kwa elimu ya sekondari na vyuo vikuu na mwelekeo huu unatazamiwa kuendelea wakati ambapo wanafunzi wengi zaidi wanatarajiwa kujiunga na vyuo vya elimu vilivyo juu ya kiwango cha shule za msingi[1] (Kielelezo 44).

## Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuhakikisha matumizi bora ya walimu pamoja na kushughulikia swala la kutokuwepo kwa walimu shuleni

**4.3** **Kenya imepiga hatua katika viwango vya upataji waelimu na uwezo wa kusoma.** Kenya ina idadi kubwa ya vijana walioelimika: Katika mwaka wa 2009, viwango vya elimu ya vijana vilikuwa juu zaidi ya nchi zingine kama vile Afrika Kusini, Ghana, Uganda na Tanzania (Jedwali 5). Katika mwaka huohuo, viwango vya usajili katika shule za msingi vilikuwa asilimia 92.9, ambavyo vilikuwa juu kidogo zaidi ya Uganda (asilimia 92.2), Afrika Kusini (asilimia 84.7), Ghana (asilimia 76.2 ) na wastani wa Nchi Zilizo Chini ya Jangwa la Sahara (asilimia 75.1). Mafanikio ya Kenya yako katika kiwango kimoja na nchi zingine zenye mapato wastani.

**Jedwali 4: Hesabu ya malipo ya wafanyikazi kwa kiwango cha juu zaidi katika jumla ya bajeti ya sekta ya elimu**

| Bajeti ya Sekta ya Elimu (Shilingi bilioni) | 2006/7 | 2007/8 | 2008/9 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Malipo ya wafanyikazi | 70.9 | 79.0 | 84.3 | 93.5 | 106.2 | 115.4 | 145.9 | 144.8 | 147.2 |
| Matumizi ya bidhaa na huduma | 2.4 | 3.8 | 7.0 | 6.9 | 7.8 | 9.9 | 16.6 | 18.3 | 18.5 |
| Ruzuku, malipo na misaada | 22.3 | 34.4 | 43.8 | 46.2 | 61.2 | 73.3 | 97.9 | 107.3 | 122.8 |
| Upataji wa rasilimali zisizo za kifedha | 0.3 | 4.1 | 4.9 | 7.9 | 9.4 | 3.7 | 5.3 | 5.8 | 6.4 |
| Jumla | 96.0 | 121.3 | 139.9 | 154.4 | 184.6 | 202.3 | 265.8 | 276.2 | 294.9 |


*Chanzo: Wizara ya Elimu ya Msingi na makadirio ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknologia 2009/10, Ripoti ya Sekta ya Elimu na Makadirio ya Matumizi ya Muda Wastani 2012/13–2014/15*

**4.4** **Kenya imewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye elimu katika miaka michache iliyopita.** Kati ya mwaka wa 2005 na 2010, jumla ya matumizi ya sekta ya elimu yalifikia wastani wa asilimia 6.4 ya Jumla ya Mapato ya Serikali—kiwango juu zaidi ya wastani wa nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara wa asilimia 3.8 ya Jumla ya Mapato ya Serikali, na pia juu zaidi ya Afrika Kusini

1 *Chanzo: Wizara ya Elimu ya Msingi na makadirio ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknologia 2009/10, Ripoti ya Sekta ya Elimu na Makadirio ya Matumizi ya Muda Wastani 2012/13–2014/15*


na Uganda (tazama Kielelezo 45). Sekta ya elimu inachangia pakubwa katika matumizi ya serikali, ikigharimu asilimia 30 ya matumizi ya kawaida ya bajeti. Mgawo wake uliongezeka kwa asilimia 28 katika mwaka wa 2005 hadi mwaka wa 2011. Hii inathibitisha kujitolea kwa serikali katika uwekezaji katika uelimishaji wa wanachi wa Kenya.

**Kielelezo 43: Kuongeza mgawo kwa ajili ya elimu ya bure ya sekondari**




*Chanzo: Hesabu ya makadirio ya KENAO*

**Kielelezo 44: Ulinganishi wa matumizi ya sekta elimu na viwango vya elimu, 2010**




*Chanzo: Indiketa za Maendeleo ya Kidunia, 2011*

**4.5** **Hata hivyo, ikilinganishwa kimataifa, Kenya inaweza kufikia viwango vya chini vya matumizi kama nchi zingine.** Kielelezo 45 unaonyesha kwamba nchi zingine zimepata mafanikio kama haya zikitumia viwango vidogo vya matumizi. Hii inamaanisha ya kwamba Kenya haina budi kutafuta njia zingine za kuongeza viwango vya matumizi bora kwa sababu ya shinikizo za kifedha zilizoko kama tulivyoona awali katika Sehemu ya 3. Sehemu zifuatazo zinatoa maelezo zaidi ya jambo hili.

**4.6** **Hata hivyo, uwekezaji mkubwa katika sekta ya elimu umeboresha sana usambazaji wa pembejeo za elimu.** Utafiti kutoka kwa Indiketa ya Utoaji Huduma (SDI) za Elimu[2] kwa shule za msingi nchini Kenya katika mwaka wa 2012 unaonyesha kwamba asilimia 98 ya pesa za elimu bure ya msingi hufikia shule zilizotengewa pesa hizo kwa kuimarisha pembejeo muhimu za elimu. Kwa

*2 Huu ni uchunguzi unaowakilisha utafiti wa kitaifa wa shule za msingi za umma pamoja na kufuatilia matumizi ya pesa za umma katika elimu na pia viwango vinavyolengwa ili kuboresha huduma za elimu huku mkazo ukitiwa katika bidii na ujuzi wa watoaji wa huduma za elimu shuleni.*

**Jedwali 5: Indiketa muhimu za elimu kwa mataifa kadhaa (2009)**

| Indiketa | Kenya | Tanzania | Uganda | South Africa | Egypt | Ghana | Mauritius | Sub-Saharan Africa | High income: OECD |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiwango cha elimu, jumla ya vijana (asilimia ya watu wenye umri kati ya 15-24) | 92.7 | 77.4 | 87.0 | 88.7 | | 80.1 | 96.5 | 71.9 | 99.7 |
| Kiwango cha ukamilishaji wa elimu ya msingi, jumla (asilimia ya umri unaohusika) | 83.2 | 102.3 | 72.8 | 93.2 | 96.0 | 82.7 | 89.4 | 66.9 | 98.4 |
| Uwiano wa wanawake kwa wanaume waliosajiliwa katika elimu ya msingi (asilimia) | 97.7 | 100.0 | 101.3 | 96.0 | 95.8 | 99.0 | 100.1 | 91.6 | 100.0 |
| Uwiano wa wanawake kwa wanaume waliosajiliwa katika elimu ya sekondari (asilimia) | 90.4 | 78.4 | 83.7 | 104.9 | 96.5 | 88.6 | 102.5 | 79.3 | 99.8 |
| Wanaorejelea, shule ya msingi, jumla (asilimia ya jumla ya viwango vya kusajiliwa) | - | 2.4 | 11.7 | 8.0 | 3.3 | 6.5 | 3.7 | 10.9 | 0.4 |
| Viwango vya usajili shuleni, shule za msingi (asilimia halisi) | 92.9 | 96.4 | 92.2 | 84.7 | 95.4 | 76.2 | 94.0 | 75.1 | 95.6 |
| Matumizi ya pesa za umma, jumla (asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali) | 6.4 | 3.6 | 3.2 | 5.4 | - | - | 3.2 | 3.8 | - |

*Chanzo: Indiketa za Maendeleo ya Kidunia, UN Malengo ya Milenia na ripoti za serikali*

sababu ya pembejeo hizi, viwango vya elimu ya Kenya sasa vinalingana vizuri na viwango muhimu katika nchi zingine, kama vile Tanzania na Senegali. Kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 6, uwiano wa wastani wa mwanafunzi kwa vitabu wa wanafunzi 3:1 wakitumia kitabu kimoja si tofauti sana na kiwango cha juu zaidi kilichotengwa na serikali cha 3:0. Uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu na wanafunzi kwa darasa ni bora kuliko malengo ya kitaifa. Indiketa ambayo haikuwa na matokeo bora ni usafi shuleni ambapo asilimia 31 ya shule za umma bado hazina vyoo bora. Utafiti huu unaonyesha ya kwamba kwa jumla, matumizi katika sekta ya elimu yamechangia katika kuboresha kwa indiketa za pembejeo za elimu.

**Jedwali 6: Ulinganishi wa pembejeo za elimu kwa viwango vya kitaifa**


| Pembejeo | Indiketa ya Maendeleo ya Kenya | Malengo ya Viwango vya Kenya | Malengo ya Viwango vya Tanzania | Malengo ya Viwango vya Senegali |
|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi kwa kila darasa | 31 | 45 | 74 | 34 |
| Uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu | 33:1 | 40:1 | 49:1 | 29:1 |
| Uwiano wa wanafunzi kwa kitabu (darasa la nne) | 3.1 | 3.0 | | |
| Uwepo wa rasilimali za ufundishaji | 95 | 100 | | |
| Mgawo wa elimu bure ya msingi ufikiao shule (Shilingi kwa kila mwanafunzi) | 988 | 1,020 | | |

*Chanzo: Kenya PETS++ 2012, Malengo ya Viwango vya Maendeleo ya Tanzania 2010, Malengo ya Viwango vya Maendeleo ya Senegali, 2010*

## Mtazamo wa Ubora

**4.7 Licha ya viwango vya juu vya matumizi na uimarishaji wa pembejeo shuleni, matokeo ya elimu yamezidi kuwa duni.** Kwa mfano, ni asilimia 36 tu ya wanafunzi wa darasa la tatu wanaoweza kufuzu katika mtihani wa hesabu wa darasa la pili na matokeo ya kufuzu ni asilimia 55 tu ya wanafunzi wa darasa la nne. Hata hivyo, matokeo haya ni bora zaidi kuliko nchi ya Uganda (asilimia 25) na Tanzania (asilimia 18 kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 46).

**Kielelezo 45: Asilimia ya wanafunzi wanaoweza kufuzu katika mtihani wa hesabu wa darasa la pili**





*Chanzo: Je Watoto Wetu Wanaelimika? Ripoti ya Shirika la Uwezo, 2011*

**4.8 Ripoti ya utafiti wa Julai 2012 (Kenya PETS++/Ripoti ya Indiketa za Maendeleo)** zaonyesha asilimia 42 tu ya wanafunzi wote wa darasa la 4 na asilimia 28 ya wanafunzi katika shule za msingi za umma wangeweza kusoma hadithi ya kiwango cha darasa la tatu (wakisoma sahihi karibu maneno 52 ya maneno 58 kwenye hadithi fupi), na asilimia 56 tu na asilimia 64 ya wanafunzi wa darasa la nne wangefuzu katika hesabu moja la kuzidisha au kugawa tarakimu moja. Matokeo duni kama haya yanahusishwa na ukosefu wa pembejeo za kutosha ama huduma duni za watoaji elimu. Matokeo kutoka kwa ripoti ya PETS++/Indiketa

ya Maendeleo ya Elimu yaliyoonyeshwa katika Jedwali 6 yanathibitisha kwamba utoaji pembejeo husaidia kufikia viwango vinavyolengwa. Hii inamaanisha kwamba ukosefu wa ubora kwa watoaji na ukosefu wa ubora katika matumizi ya pembejeo za elimu huchangia pakubwa katika mtafaruku kati ya matumizi ya elimu na matokeo ya elimu. Ukosefu wa ubora wa kiufundi katika utoaji huduma katika elimu ndiyo changamoto kubwa kuliko ukosefu wa ubora kati mgawo.

4.9 **Vyanzo viwili vinavyoleta ukosefu wa huduma bora katika sekta ya elimu nchini ni kutohudhuria shule kwa walimu na huduma duni/ukosefu wa maarifa kwa walimu.** Sehemu kubwa ya walimu hukosekana darasani. Utafiti wa Maendeleo katika sekta waonyesha kwamba wastani wa asilimia 16 ya walimu wa shule za msingi walikosekana shuleni wakati walipohitajika shuleni na kati ya wale waliojitokeza, asilimia 32 (yaani asilimia 27 ya walimu wote) hawaendi darasani wakati wanapohitajika. Kwa hivyo, ni asilimia 55 tu ya walimu ambao huwa darasani wakati unaofaa (Tazama Kielelezo 47). Kuzidisha shida, thuluthi mbili ya walimu hukosa ujuzi wa kufunza na uzoefu wa kufunza kulingana na matakwa ya silabasi ya viwango vya chini vya hesabu na somo la Kiingereza katika shule za msingi. Walimu hawakufuzu vyema katika ujuzi wa kufunza kwani walipata wastani wa asilimia 36 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 65 kwa somo la Kiingereza na asilimia 82 katika somo la Hesabu. Hii inaonyesha kwamba changamoto kubwa zilizo katika sekta ya elimu ziko kwa huduma na bidii ya walimu kuliko katika kupatikana kwa miundo misingi (pembejeo za shule).

**Kielelezo 46: Mahali walipopatikana walimu wakati wa uchunguzi**




*Chanzo: Kenya PETS++, 2012*

4.10 **Kuongeza matumizi kwa kuajiri walimu zaidi hakutasaidia sana ikiwa walimu walioajiriwa tayari hawaendi darasani kufunza.** Wanafunzi hufunzwa kwa muda wastani wa asilimia 55 ya muda wote wanaotakikana kufunzwa tukizingatia ukosefu wa walimu shuleni na darasani. Hii inamaanisha pia kwamba ukosefu wa walimu shuleni husababisha uwiano mkubwa wa uongo kati ya mwanafunzi na mwalimu (uwiano wa mwanafunzi kwa

mwalimu wa 41:3 ukilinganishwa na 33 kwa misingi ya ujumla wa idadi ya walimu shuleni) kumaanisha kwamba ukosefu unaongeza wanafunzi saba zaidi kwa kila mwalimu. Kwa hivyo, ijapokuwa makadirio ya bajeti ya mwaka 2011/12 yalijumlisha Shilingi bilioni 118.7 zilizotengewa mishahara ya walimu, ikijumlisha kuajiriwa kwa walimu wapya 10,000 katika mwaka wa 2011/12, mabadiliko mema katika matokeo ya elimu yanaweza yasionekane ikiwa walimu wataendelea kukosa shule kwa kiwango cha juu.

4.11 **Faida itapatikana kutokana na mipango inayolenga kuwashinikiza walimu watumie muda wingi darasani.** Ukosefu wa walimu darasani hupoteza rasilimali za kibinadamu za asilimia 47 (tazama Jedwali 7) ya jumla ya matumizi kwa mishahara ya walimu. Viwango vikubwa vya ukosefu katika shule za umma huongeza gharama ya kufunza shuleni kwa saa moja kwa kiwango cha asilimia 51 kwenye shule za umma ikilinganishwa na shule za kibinafsi. Hii inaonyesha usimamizi mbaya katika shule za umma—matokeo yanayokubaliana na utafiti kwamba wakuu wa shule wana uzekano maradufu wa kukosekana shuleni kuliko walimu wa kawaida na walimu walioajiriwa na serikali walikosa shule kwa asilimia 50 kuliko walimu walio katika vibarua (tazama Kielelezo 48). Hii inamaanisha kwamba utoaji hesabu na utathmini wa utendakazi ni duni katika viwango vya shule. Kutia nguvu utoaji hesabu na kutoa zawadi na kutoa adhabu ni muhimu ili sekta ya elimu ipate faida.

**Jedwali 7: Viwango vya kukosekana shule kulingana na aina ya shule**

| Indiketa | Zote | Za Umma | Za Kibinafsi |
|---|---|---|---|
| Asilimia ya walimu waliokosekana shule | 0.16 | 0.16 | 0.13 |
| Asilimia ya walimu walioenda shuleni lakini hawakwenda darasani | 0.32 | 0.38 | 0.20 |
| Asilimia ya walimu waliokosekana darasani (hawakuwa shuleni ama darasani) | 0.42 | 0.47 | 0.31 |
| Darasa lenye wanafunzi lakini bila mwalimu | 0.31 | 0.36 | 0.19 |
| Muda uliotumika kufunza (kwa saa 5 na dakika 40 ya muda uliotengwa) | 2 hr 40 min | 2 hr 19 min | 3 hr 38min |

*Chanzo: Kenya PETS++, 2012*


4.12 **Shida ya ukosefu wa walimu bora ni shida kubwa zaidi inayosabisha shida za kiufundi. Hakuna budi kuwa na mabadiliko ya mwelekeo ya matumizi ya pesa za elimu kutoka si wingi tu wa pembejeo bali ubora wa pembejeo.** Ijapokuwa uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu uliimarika, zaidi ya nusu ya walimu walikosa maarifa ya kiwango kidogo kabisa ya kufunza somo la Hesabu na somo la Kiingereza katika viwango vya chini vya shule za umma. Walimu wa Hesabu walichukia sana kufunza tarakimu isiyo kamili na waliofunza Kiingereza

walichukia sana kufunza insha (Kielelezo 49). Walimu wote hawakufuzu vizuri katika ujuzi wa ufundishaji. Maarifa haya duni ya walimu hupunguza nguvu za mshikamano kati ya elimu na matokeo yake. Shida hii haiwezi kusuluhishwa kwa kuajiri walimu wapwa ili kuongeza idadi yao. Linalotakikana ni kuezeka katika kufunza walimu, kujenga uwezo wao na kuboresha usimamizi wa shule ili kutia walimu motisha .

4.13 **Ubora wa elimu ya chekechea nchini Kenya katika shule za umma hauzingatii ufunzaji mwema wa mapema na pia lishe bora.** Mbinu za ufundishaji zinazolenga uwezo wa motto, ambazo zingesaidia sana uelewa wa watoto, zinapatikana tu shuleni chache za kibinafsi tena katika miji mikubwa.


4.14 **Usajili wa wanafunzi katika vyuo vikuu umekua maradufu katika miaka mine iliyopita lakini ni vizuri pia changamoto za ubora wa utaratibu wa elimu ya vyuo vikuu ushughulikiwe na pia mshikamano wake na matakwa waajiri.** Pana viwango vikubwa vya ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana, na pia vijana wengi wana viwango vya chini vya

**Kielelezo 47: Uwezekano wa kukosekana shuleni**




*Source: Kenya PETS++ 2012*
*Note: This is probability of absenteeism controlling for other teacher characteristics, making this a comparison among teachers with similar characteristicsexcept for either the position or appointment type.*

**Kielelezo 48: Matokeo ya walimu wa shule za umma katika kujua silabasi na ujuzi wa kufunza**




*Chanzo: Utafiti wa Kenya PETS++, 2012*

elimu. Vijana wengi wameajiriwa katika sekta ya Kilimo, wanapata mshahara kidogo na hawawezi kupata huduma za kijamii kama vile huduma za afya na nyumba bora za kuishi. Sekta ya vyuo na masomo ya kiufundi (TVET) pia inakumbana na changamoto nyingi zikiwemo masomo yaliyo gawanyika sehemusehemu badala ya kuwa pamoja, kukosa mshikamano na sekta ya elimu ya kawaida, ukosefu wa mshikamano na waajiri, ukosefu wa fedha, ukosefu wa usimamizi bora, nafasi za kazi lakini zenye mishahara midogo za wenye digrii katika sekta hii na ukosefu wa mshikamano kati ya uvumbuzi wa kiufundi nchini na soko la kimataifa.


## Mtazamo wa Usawa

**4.15 Usajili katika viwango vyote vya elimu umeongezeka kwa muda mchache uliopita lakini ubora wa huduma za sekta ya elimu na tofauti kubwa ya kimaeneo bado ni changamoto kubwa.** Usajili na kuendelea kukaa shuleni, hasa kwa wasichana katika shule za msingi katika maeneo kame kuko katika kiwango kidogo sana. Ijapokuwa matokeo ya wanafunzi wa darasa la sita katika mitihani ya Hesabu na Kusoma ni bora kuliko nchi nyingine katika nchi zilizo chini ya jangwa la Sahara, jumla ya matokeo katika masomo yote iko chini na kwa hivyo wanafunzi hawaendelei vyema katika elimu yao katika viwango vyote.

**4.16 Tofauti kubwa katika matumizi kwa kila mwanafunzi katika kiwango cha kaunti inaweza kuelezwa na tofauti za walimu wanavyo patikana kimaeneo.** Fauka ya hayo, ijapokuwa matumizi kwa kila mwanafunzi yanatofautiana, kaunti zingine zina ubora wa hali ya juu kwa matumizi mema na pia matokeo mema. Kwa mfano, pamoja na matumizi ya chini kwa kila mwanafunzi katika shule za msingi, Samburu na Turkana zina uwiano bora wa mwalimu kwa wanafunzi kupita Wajir na Tana River (Kielelezo 50).

**4.17 Usawa ni changamoto kubwa katika sekta ya elimu ya Kenya, ijapokuwa malengo ya kitaifa ya pembejeo katika elimu yametimia.** Matokeo kutoka kwa utafiti wa PETS++/SDI yanaonyesha kwamba zaidi ya asilimia 17 ya shule zina uwiano wa mwanafunzi kwa kitabu ulio mkubwa zaidi ya 4, na wastani wa wanafunzi wanaotumia kitabu kimoja ukiwa maradufu huko Nyandarua na Siaya kuliko Nairobi (tazama Jedwali 8). Pia ndivyo mambo yalivyo katika uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu, ambao pia waonyesha utofauti mkubwa wa kimaeneo. Ongezeko la matumizi katika sekta ya elimu halina budi kulengwa katika kuongeza usawa wa upatikanaji wa pembejeo shuleni na si ongezeko la jumla kwa pembejeo za elimu.

**Kielelezo 49: Tofauti kubwa katika uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi katika viwango vya kaunti**




*Chanzo: Wizara ya Afya, 2012*
*Teacher-pupil ratio in public schools – Uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi katika shule za umma*

**4.18 Bajeti na kutengwa kwa rasilimali katika siku za usoni zilengwe katika kusuhulishwa changamoto za usawa katika utoaji wa pembejeo.** Ijapokuwa asilimia wastani ya pesa za elimu bure ya msingi zinazofikia shule ni kiwango cha asilimia 97 ya pesa zote zilizotengwa, wastani wa wale waopata chini ya asilimia 95 ya pesa hizo ni asilimia 80. Fauka ya hayo, sehemu kubwa ya shule hupata pesa nyingi zaidi ya inavyohitajika. Hii inadhihirishwa na asilimia 25 ya shule za umma zilizo ripoti kupokea asilimia 10 ama zaidi za mgao wa pesa hizo zaidi ya usajili wao wa wanafunzi, japo asilimia 16 ya shule zilipata chini ya asilimia 80 ya pesa zilizotakiwa kupata. Kwa sababu pesa za elimu bure ya msingi hupitia akaunti za bengi za shule, tofauti kubwa za mgawo huo huletwa na mtafaruku kati ya idadi ya usajili inayotumiwa kutenga pesa hizo na idadi kamili ya wanafunzi wanaosajiliwa shuleni. Tathmini

**Jedwali 8: Ulinganishi wa pembejeo za shule kulingana na kaunti**

| Mahali | Uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu | Uwiano wa mwanafunzi kwa kitabu |
|---|---|---|
| National | 33.1 | 3.1 |
| Nairobi | 42.1 | 2.1 |
| Nyamira | 29.4 | 3.1 |
| Nyandaura | 39.3 | 4.4 |
| Siaya | 33.5 | 4.0 |

*Chanzo: Utafiti wa Kenya PETS++, 2012*

za hesabu za usajili kwa ajili ya mpango wa elimu bure ya msingi na nyongeza ya pesa hizi kulingana na mahitaji vinahitajika ili kuweza kufikia lengo la usawa katika muktadha wa ubanifu wa fedha katika bajeti.

**4.19 Mipango katika sekta ya elimu na tathmini ya data vimetawanyika na kungekuwa na faida kubwa kama kungewekwa mipango kabambe katika sekta hiyo, kuboreshwa kwa usimamizi wa pesa za umma na uratibu mwema kati ya serikali ya kitaifa na zile za kaunti, kukiwemo kupanuliwa kwa miundo misingi.** Hali ilivyo sasa malengo ya kitaifa ya sekta ya elimu hayatafsiriwi kuwa malengo ya wilaya, na kinyume chake; na tathmini ya ubora ya mfumo mzima inakosekana katika sekta hii.

Sura ya 5

# TAMATI

5.1 **Muongo wa kudumisha nidhamu ya kifedha na usimamizi wa uchumi umeanza kuzaa matunda.** Utumizi wa rasilimali za kitaifa umeongezeka sana katika rasilimali zilizotengewa miundo misingi hasa barabara, kawi, wanja za ndege na teknologia ya habari na mawasiliano. Uwekezaji katika rasilimali za kibinadamu unaonekana katika ongezeko la viwango vya uwezo wa kusoma na kuandika, ambavyo sasa vimefikia viwango vya mataifa yenye mapato kadri. Kwa bahati mbaya, habari za sekta ya afya zavunja moyo zaidi. Akina mama wengi bado wanaaga dunia wakati wa kujifungua, viwango vya vifo vya watoto na wale wenye umri chini ya miaka mitano bado viko juu na uboreshaji wa kupatikana kwa maji safi bado ni changamoto. Sekta hizi zahitaji kushughulikiwa kwa haraka.

5.2 **Uboreshaji wa matumizi ya fedha utasaidia kupata fedha zaidi za matumizi mengine bila kuongeza deni la serikali.** Kenya sasa yaweza kupata rasilimali za kutosha ili kukidhi mahitaji yake ya kimaendeleo. Hata hivyo, shinikizo zinazochipuka za kifedha kutokana na madai ya nyongeza za mishahara, viwango viwili vya serikali vilivyoletwa na ugatuzi na taasisi za kikatiba vitahitaji nidhamu kubwa zaidi ya kifedha. Shinikizo hizi mpya zitatengeneza nafasi ya kuboresha utendakazi na kupunguza matumizi mabaya ya fedha katika shughuli za serikali. Sekta ya elimu yaweza kutumika kama mfano katika uchunguzi.

5.3 **Sekta ya elimu itavuna matunda mema kutokana na kuboresha utendakazi na matumizi mema ya rasilimalikwa sababu ya mfumo mwema wa uwajibikaji na uwazi ili kupunguza kutohudhuria kwa walimu shuleni na kupunguza gharama ya kufunza kwa saa moja.** Faida itapatikana katika sekta ya elimu kama washikadau watazingatia ubora wa walimu na kuanzisha uwazi na uwajibikaji ili kutia walimu motisha. Kuajiri walimu zaidi si suluhisho la

kuboresha matokeo katika sekta ya elimu kwa sababu ubora wa walimu wanaoajiriwa hauwezi kupuuziliwa mbali.

5.4 **Kwa wastani, malengo ya kitaifa kwa ajili ya indiketa za utoaji huduma yamefikiwa lakini tofauti za kimaeneo bado zinadumu.** Usajili katika shule za msingi, uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu na maeneo ya kufikiwa na chanjo mbalimbali ni mifano inayothibitisha vile ambavyo mafanikio ya kitaifa yanaweza kufunika unyonge wa tofauti za kimaeneo. Serikali ya ugatuzi imeundwa ili kufunika mapengo lakini mfumo wa usimamizi wa pesa za umma ulio na unyonge na mapengo yadhoofisha mpango huo.

5.5 **Mageuzi yanayoleta changamoto sana yana misingi katika sheria.** Kanuni za katiba ya mwaka wa 2010 zilileta mageuzi katika sheria za ugavi wa rasilimali pamoja na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Mageuzi katika ununuzi wa bidhaa na huduma na usimamizi wa fedha za umma pia yamekita mizizi katika sheria. Hata hivyo, sheria hizi zina umuhimu lakini hazitoshi: mafanikio katika utekelezaji wa mageuzi haya utaamua kwa sehemu kubwa mafanikio ya ugatuzi nchini Kenya. Lengo kuu ni kujenga uwezo wa taasisi na mashirika yatakayo telekeleza hasa wizara mbalimbali na serikali za kaunti.

# VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho 1: Bajeti ya 2009/10 – 2012/13

| | 2011/12 | 2012/13* | 2013/14** | 2014/15** |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA MAPATO** | **748** | **955** | **987** | **1,139** |
| Mapato yatakayogawanywa | 690.7 | 850 | 920 | 1,063 |
| **MATUMIZI NA FEDHA ZILIZOTOLEWA** | **948** | **1,263** | **1,374** | **1,407** |
| Matumizi ya kawaida | 647 | 805 | 855 | 909 |
| Kitaifa | | 667 | 752 | 854 |
| Kaunti | | 186 | 207 | 208 |
| Matumizi ya maendeleo na fedha zilizotolewa | 301 | 447 | 507 | 482 |
| Upungufu (pesa taslimu ikiwemo misaada) | -184 | -251 | -319 | -193 |
| **Misaada** | 15 | 56.2 | 67 | 76 |
| FEDHA | 172 | 251 | 319 | 193 |
| Fedha kutoka ng'ambo | 99 | 144 | 213 | 101 |
| Fedha kutoka nchini | 73 | 107 | 107 | 93 |
| Fedha zilizokopwa kutoka nchini | 73 | 107 | 107 | 93 |
| Zingine (zikiwemo kutoka kwa kuuza mali umma) | - | - | - | - |
| Jumla ya Mapato ya Serikali (Shilingi bilioni) | 3,306 | 3,867 | 4,165 | 4,775 |
| Jumla ya deni (ya umma + ya kibinafsi nje ya nchi), Dola za Marekani bilioni | 17 | 20 | 24 | 25 |
| Jumla ya Mapato ya Serikali (Dola za Marekani bilioni, bei za sasa) | 41 | 46 | 49 | 56 |
| Kiwango cha ukuaji cha Jumla ya Mapato ya Serikali | 4 | 5 | 6 | 6 |
| Kiwango cha ongezeko la watu | 3 | * | * | * |
| GDP per capita (Dola za Marekani) | 808 | * | * | |
| **Mgawo kwa Jumla ya Mapato ya Serikali (asilimia)** | | | | |
| Mapato | 23 | 25 | 24 | 24 |
| Matumizi | 29 | 33 | 30 | 30 |
| Pengo la upungufu | -6 | -7 | -5 | -4 |
| Jumla ya Deni (la umma + la kibinafsi nje ya nchi) | 45.7 | 45.8 | 45.8 | 44.2 |


*Chanzo: Ripoti kadhaa za QBER, Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Indiketa za Maendeleo ya Kidunia 2012*

**Kiambatanisho 2: Makadirio ya bajeti ya sekta mbalimbali, Shilingi bilioni**

| | 2002/03 | 2003/04 | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Maendeleo ya Rasilimali za Kibinadamu | 87.9 | 100.2 | 107.6 | 128.1 | 140.0 | 141.3 | 152.1 | 177.5 |
| Miundo misingi | 30.0 | 31.9 | 37.5 | 52.9 | 73.9 | 104.5 | 124.2 | 151.2 |
| Utawala, Haki, Sheria na Taratibu | 43.2 | 46.9 | 53.5 | 64.6 | 58.3 | 69.0 | 72.9 | 85.3 |
| Usimamizi wa Sekta ya Umma na Uhusiano wa Kimataifa | 25.4 | 26.3 | 42.1 | 41.7 | 61.1 | 96.2 | 61.7 | 72.9 |
| Mazingira, Maji na Unyunyiziaji | 7.0 | 9.7 | 9.4 | 11.6 | 15.8 | 23.6 | 31.9 | 39.3 |
| Mipango Maalum | 1.9 | 2.8 | 2.6 | 3.5 | 15.1 | 17.3 | 35.9 | 33.1 |
| Utafiti, Uvumbuzi na Teknolojia | - | - | 0.7 | 1.1 | 5.8 | 21.7 | 26.0 | 30.1 |
| Kilimo na Maendeleo ya Maeneo ya Mashambani | 11.4 | 12.0 | 14.0 | 16.5 | 21.5 | 28.6 | 29.0 | 30.0 |
| Biashara, Utalii na Viwanda | 4.1 | 4.6 | 6.0 | 6.1 | 9.5 | 7.1 | 8.2 | 12.0 |
| Usalama wa Kitaifa | 3.5 | 3.9 | 4.2 | 5.2 | 6.0 | 8.2 | 7.7 | 10.1 |
| Jumla (Kuacha nje matumizi ya ulinzi) | 214.3 | 238.3 | 277.6 | 331.2 | 407.1 | 517.4 | 549.5 | 641.5 |


*Chanzo: Makadirio yaliyochapishwa (miaka mbalimbali)*


**Kiambatanisho 3: Tofauti kati ya mapato hasa na viwango vilivyolengwa**





*Chanzo: Hesabu iliyofanywa na wafanyikazi wa Shirika la Kutoza Ushuru Nchini (KRA) 2012*

**Kiambatanisho 4: Ongezeko la thamani ndogo za ushuru zikilinganishwa na misingi yake**




*Chanzo: Hesabu iliyofanywa na wafanyikazi wa Shirika la Kutoza Ushuru Nchini (KRA) 2012*

### Kiambatanisho 5: Pendekezo la Kodi ya Nyongeza ya Thamani 2012

| | Bidhaa na huduma zisizo chini ya Mswada wa Kodi ya Nyongeza ya Thamani Sura 476 | Bidhaa na huduma zisizo chini ya Mswada wa Kodi ya Nyongeza ya Thamani, 2012 |
|---|---|---|
| Bidhaa na huduma zisizo chini ya mwada huu | Bidhaa: Kuku, mifugo (nyama na maziwa ambazo hazijapitishwa kwenye mtambo), samaki mbichi na vyakula vingine vitokavyo baharini, bidhaa za ukulima zisizopitishwa kwenye mtambo, bidhaa za petroli, fedha za kigeni, makaa, silaha za vita, visodo, ngozi mbichi, filamu za sinema, nafaka na unga uliotengenezwa kwa nafaka | Bidhaa: Pembejeo za ukulima, bidhaa za petrol, bidhaa za maabara, wanyama hai, maziwa ambayo hayajapitishwa kwa mtambo, mayai, nyama, matunda na njugu, mashine, nafaka isipokuwa mahindi, ngano na shayiri |
| | Huduma: Zisizotozwa ni huduma za kifedha, bima, elimu ya umma na huduma za mafunzo, huduma za afya (ikiwemo ya mifugo), huduma za usafi, huduma za kilimo, uchukuzi, mazishi na huduma za kuchoma maiti, kukodisha na kupangisha ardhi na nyumba, huduma za posta na huduma za kijamii | Huduma: Zisizotozwa ni huduma za kifedha, bima, elimu ya umma na huduma za mafunzo, huduma za afya (ikiwemo ya mifugo), huduma za usafi, huduma za kilimo, uchukuzi, mazishi na huduma za kuchoma maiti, kukodisha na kupangisha ardhi na nyumba, huduma za posta na huduma za kijamii |
| Bidhaa na huduma zinazotozwa katika kiwango cha sufuri (0) | Bidhaa: Maziwa, mchele, unga wa mahindi na ngano, pembejeo za ukulima, dawa na vifaa vya hospitali, mafuta taa na gesi ya kupikia, dawa za kuua wadudu, magazeti na majarida, mashine za kilimo na vipuri vyake, genereta, mashine ya kutengeneza nguo pamoja na vipuri vyake, ambulensi, vifaa vya elimu, ununuzi wa magari ya umma | Bidhaa: Dawa na vifaa vya kusambazia dawa |
| | Huduma: Biasharanje, huduma safarini, upelekaji wa majani na kahawa kwa biasharanje, usambazaji wa nguvu za umeme nyumbani (<200KW), huduma za wanja za ndege, uchimbaji maji | Huduma: Biasharanje, usafiri kwa ndege wa kimataifa, usambazaji bidhaa zinazotengenezwa na kampuni za EPZ, huduma za usambazaji na usafi wa maji na usambazaji wa kahawa na majani ya kuuza kwa mnada |

*Chanzo: Mswada wa Kodi ya Nyongeza ya Thamani, 2012*

### Kiambatanisho 6: Fomyula ya kukadiria kielezo cha kodi kinavyokabiliana na kupanda kwa pato la taifa

Generally, the elasticity concept assumes the following functional relationship:

$$T = \alpha B^{\beta} \varepsilon$$

Where T = tax revenue, B = Tax base, a and β represent parameters to be estimated, and ε is the multiplicative error term. Taking logs, we obtain a log-linear specification of the form:

$$LogT = Log\alpha + \beta LogB + Log\varepsilon$$

This equation can be presented in the following standard form:

$$LogT_t = \alpha + \beta LogB_t + \mu_t$$

When using unadjusted revenue data, the coefficient β represents the tax buoyancy of the tax revenue to its base.

### Estimation of long run tax revenue buoyancy

| Variable | Coefficient | Std. Error | t-Statistic | Prob. |
|---|---|---|---|---|
| **Real gross domestic product (log)** | **1.26** | **0.04** | **33.18** | **0.00** |
| Dummy 2004 | -0.17 | 0.06 | -2.91 | 0.01 |
| Dummy 2001 | -0.15 | 0.06 | -2.53 | 0.02 |
| Dummy 2000 | -0.12 | 0.06 | -2.14 | 0.04 |
| Constant | -5.12 | 0.52 | -9.89 | 0.00 |
| R-squared | 0.98 | | | |
| Adjusted R-squared | 0.97 | | | |
| Prob(F-statistic) | 0.00 | | | |

*Source: Printed estimates (various years)*

### Estimation of short run tax revenue buoyancy

| Variable | Coefficient | Std. Error | t-Statistic | Prob. |
|---|---|---|---|---|
| **Total revenue (log, 1st difference, 1st lag)** | **0.32** | **0.27** | **1.19** | **0.26** |
| Total revenue (log, 1st difference, 2nd lag) | 0.14 | 0.23 | 0.61 | 0.55 |
| Total revenue (log, 1st difference, 3rd lag) | -0.06 | 0.22 | -0.28 | 0.78 |
| Total revenue (log, 1st difference, 4th lag) | 0.11 | 0.21 | 0.55 | 0.59 |
| Real gross domestic product (log, 1st difference) | 0.42 | 0.29 | 1.43 | 0.18 |
| Real gross domestic product (log, 1st difference, 1st lag) | -0.18 | 0.36 | -0.51 | 0.62 |
| Real gross domestic product (log, 1st difference, 2nd lag) | 0.77 | 0.34 | 2.29 | 0.04 |
| Real gross domestic product (log, 1st difference, 3rd lag) | -0.79 | 0.37 | -2.11 | 0.06 |
| Real gross domestic product (log, 1st difference, 4th lag) | -0.16 | 0.32 | -0.50 | 0.62 |
| Error correction term (1st lag) | -0.66 | 0.29 | -2.31 | 0.04 |
| Dummy 1994 | 0.18 | 0.05 | 3.23 | 0.01 |
| Dummy 2010 | 0.15 | 0.05 | 2.94 | 0.01 |
| Dummy 2000 | -0.13 | 0.06 | -2.37 | 0.04 |
| Constant | 0.01 | 0.02 | 0.36 | 0.72 |
| R-squared | 0.83 | | | |
| Adjusted R-squared | 0.64 | | | |
| Prob(F-statistic) | 0.01 | | | |

*Reduced Equation: total revenue (log, difference) = 0.01 + 0.105 gross value added (log,difference) + 0.18 dummy 1994 + 0.15 dummy 2010 - 0.13 dummy 2000 - 0.66 Error correction term*
*Source: Staff computations*

**Kiambatanisho 7: Sera za kifedha zimetumika kuchangamsha ukuaji wa uchumi na kuudumisha**

| Wastani 2003 - 2007 (Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali) | Wastani 2008 - 2011 (Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali) |
|---|---|
| 0.4 | 1.0 |
| 4.1 | 2.7 |
| 4.5 | 3.7 |
| 2.6 | 2.2 |
| -1.7 | -2.3 |

*Chanzo: Makadirio ya wafanyikazi wa KNBS na data ya KNBS*

**Kiambatanisho 8: Pengo kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo linapungua**

| | Matumizi ya kawaida (Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali | Matumizi ya Maendeleo na pesa zilizotolewa (Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali) |
|---|---|---|
| 1998/99 | 23 | 4 |
| 1999/00 | 20 | 2 |
| 2000/01 | 22 | 3 |
| 2001/02 | 21 | 3 |
| 2002/03 | 20 | 3 |
| 2003/04 | 20 | 3 |
| 2004/05 | 19 | 3 |
| 2005/06 | 20 | 4 |
| 2006/07 | 18 | 5 |
| 2007/08 | 21 | 7 |
| 2008/09 | 19 | 7 |
| 2009/10 | 21 | 9 |
| 2010/11 | 21 | 8 |
| 2011/12 | 19.7 | 9.1 |
| 2012/13 | 20.8 | 11.6 |

*Chanzo: Hazina ya Fedha ya Kitaifa (QEBR 2012/13) na Ripoti ya Sera ya Bajeti, 2013*

### Kiambatanisho 9: Sekta ya miundo misingi narasilimali za kibinadamu zinachukua zaidi ya asilimia 50 ya jumla ya bajeti

| | Average 2002-2005 | Average 2006-2009 |
|---|---|---|
| Maendeleo ya Rasilimali za Kibinadamu | 106.0 | 152.7 |
| Miundo Misingi | 38.1 | 113.4 |
| Utawala, Haki, Sheria na Utaratibu | 52.0 | 71.4 |
| Usimamizi wa Uongozi wa Umma na Ushirikiano wa Kimataifa | 33.9 | 73.0 |
| Mazingira, Maji na Unyunyizaji | 9.4 | 27.7 |

*Chanzo: Makadirio ya Wafanyikazi kulingana na ripoti ya Kutathmini Matumizi ya Pesa za Serikali (Kenya National Audit Office), Ripoti mbalimbali (2001/02 mpaka 2009/2010)*

### Kiambatanisho 10: Budget execution … recurrent and development

| | Makadirio yaliyobadilishwa (Shilingi bilioni) | Zilizotumika (Shilingi bilioni) | Kiwango cha Utendaji (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| **Average recurrent execution** | | | |
| 2002 - 2006 | 233.5 | 220.8 | 94.6 |
| 2007 - 2010 | 422.5 | 401.9 | 95.3 |
| **Average development execution** | | | |
| 2002 - 2006 | 82.0 | 55.5 | 66.1 |
| 2007 - 2010 | 239.1 | 180.8 | 76.3 |

*Chanzo: Makadirio ya wafanyikazi kulingana na ripoti ya Kutathmini Matumizi ya Pesa za Serikali (KENAO), ripoti mbalimbali (2001/02 mpaka 2009/2010)*

### Kiambatanisho 11: Tofauti zilizoko katika utendekazi wa bajeti, 2005 - 2010

| | Mgawo (Shilingi bilioni) | Zilizotumiwa (Shilingi bilioni) | Kiwango cha Utendakazi (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| **Maendeleo ya Rasilimali za Kibinadamu** | | | |
| 2005/06 | 128.1 | 116.4 | 90.9 |
| 2006 - 2010 | 152.7 | 144.8 | 94.8 |
| **Miundo Misingi** | | | |
| 2005/06 | 52.9 | 39.4 | 74.4 |
| 2006 - 2010 | 113.4 | 91.0 | 80.2 |
| **Utawala, Haki, Sheria na Utaratibu** | | | |
| 2005/06 | 64.6 | 56.8 | 88.1 |
| 2006 - 2010 | 71.4 | 63.7 | 89.3 |

*Chanzo: Makadirio ya wafanyikazi kulingana na ripoti ya Kutathmini Matumizi ya Pesa za Serikali (KENAO), ripoti mbalimbali (2001/02 mpaka 2009/2010)*

**Kiambatanisho 12: Pengo la mapato ambalo limedumu tangu mwaka wa 2008/09, Shilingi milioni**

| | 2002/03 | 2003/04 | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kodi ya Maduhuli | 1,563 | 274 | 1,757 | 344 | 373 | 203 | 245 | 579 | 3,121 | 3,656 |
| Kodi ya bidhaa | 2,397 | 630 | 1,951 | 2,158 | 3,969 | 1,409 | 2,181 | 848 | 4,489 | 6,236 |
| Kodi ya Nyongeza ya Thamani ya Maduhuli | 2,135 | 1,343 | 4,170 | 1,276 | 3,806 | 1,642 | 2,491 | 9,734 | 6,058 | 145 |
| Kodi ya mapato | 137 | 614 | 436 | 696 | 77 | 1,082 | 1,058 | 1,438 | 65 | 284 |
| Jumla | 2,142 | 8,477 | 33,338 | 3,370 | 4,105 | 9,244 | 12,306 | 10,825 | 6,309 | 25,994 |

*Chanzo: Shirika la Kutoza Ushuru Nchini*

**Kiambatanisho 13: Kupungua kwa misaada ya wafadhili**

| Miaka | Jumla ya Mapato ya Serikali (Dola za Marekani, milioni) | Msaada Kamili wa Wafadhili (Dola za Marekani, milioni) | Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali |
|---|---|---|---|
| 1960-1979 | 2,216 | 98 | 2.7 |
| 1980 | 7,265 | 395 | 5.4 |
| 1981 | 6,854 | 448 | 6.5 |
| 1982 | 6,432 | 485 | 7.5 |
| 1983 | 5,979 | 396 | 6.6 |
| 1984 | 6,191 | 408 | 6.6 |
| 1985 | 6,135 | 427 | 7.0 |
| 1986 | 7,239 | 443 | 6.1 |
| 1987 | 7,971 | 557 | 7.0 |
| 1988 | 8,355 | 832 | 10.0 |
| 1989 | 8,272 | 1,060 | 12.8 |
| 1990 | 8,591 | 1,181 | 13.8 |
| 1991 | 8,152 | 916 | 11.2 |
| 1992 | 8,221 | 883 | 10.7 |
| 1993 | 5,752 | 914 | 15.9 |
| 1994 | 7,148 | 677 | 9.5 |
| 1995 | 9,046 | 732 | 8.1 |
| 1996 | 12,046 | 595 | 4.9 |
| 1997 | 13,116 | 449 | 3.4 |
| 1998 | 14,093 | 415 | 2.9 |

**Kiambatanisho 13: Kupungua kwa misaada ya wafadhili**

| Miaka | Jumla ya Mapato ya Serikali (Dola za Marekani, milioni) | Msaada Kamili wa Wafadhili (Dola za Marekani, milioni) | Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali |
|---|---|---|---|
| 1999 | 12,896 | 310 | 2.4 |
| 2000 | 12,691 | 513 | 4.0 |
| 2001 | 12,987 | 471 | 3.6 |
| 2002 | 13,149 | 393 | 3.0 |
| 2003 | 14,904 | 523 | 3.5 |
| 2004 | 16,096 | 660 | 4.1 |
| 2005 | 18,738 | 759 | 4.1 |
| 2006 | 22,504 | 947 | 4.2 |
| 2007 | 27,237 | 1,327 | 4.9 |
| 2008 | 30,519 | 1,366 | 4.5 |
| 2009 | 30,580 | 1,776 | 5.8 |
| 2010 | 32,198 | 1,629 | 5.1 |

*Chanzo: Mahesabu ya Shirika la OECD na Indiketa za Maendeleo ya Kidunia, 2012*

**Kiambatanisho 14: Ulinganishi wa matumizi ya elimu na viwango vya kusoma na kuandika**

| Nchi | Matumizi ya pesa za umma katika elimu, jumla (Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali) | Kiwango cha kusoma na kuandika, jumla ya vijana (Asilimia ya vijana kati ya umri wa 15-24) |
|---|---|---|
| Algeria | 4.3 | 91.0 |
| Botswana | 8.3 | 94.6 |
| Burkina Faso | 4.5 | 34.5 |
| Burundi | 5.2 | 75.0 |
| Cameroon | 3.0 | 83.1 |
| Cote D'Ivoire | 4.3 | 63.6 |
| Egypt, Arab Rep. | 4.3 | 84.9 |
| Ethiopia | 4.5 | 47.3 |
| Gambia, The | 2.7 | 59.0 |
| Ghana | 5.4 | 75.4 |
| Guinea | 2.3 | 53.8 |
| High Income: OECD | 5.3 | 99.6 |
| Indonesia | 3.0 | 98.3 |

**Kiambatanisho 14: Ulinganishi wa matumizi ya elimu na viwango vya kusoma na kuandika**

| Nchi | Matumizi ya pesa za umma katika elimu, jumla (Asilimia ya Jumla ya Mapato ya Serikali) | Kiwango cha kusoma na kuandika, jumla ya vijana (Asilimia ya vijana kati ya umri wa 15-24) |
|---|---|---|
| Kenya | 6.3 | 86.5 |
| Lesotho | 13.4 | 91.4 |
| Liberia | 2.8 | 73.4 |
| Nchi Zenye Mapato ya Chini | 3.5 | 69.6 |
| Nchi Zenya Mapato ya Wastani | 3.5 | 81.5 |
| Madagascar | 3.2 | 67.6 |
| Malawi | 4.7 | 86.5 |
| Malaysia | 6.1 | 97.9 |
| Mauritius | 3.7 | 95.5 |
| Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Africa (mataifa yanayoendelea pekee) | 5.0 | 87.6 |
| Mataifa Yenye Mapato Wastani | 4.0 | 89.5 |
| Moldova | 6.8 | 99.5 |
| Mozambique | 4.9 | 66.4 |
| Niger | 3.4 | 25.3 |
| Philippines | 2.9 | 96.0 |
| Rwanda | 4.2 | 77.4 |
| Senegal | 4.2 | 55.0 |
| Seychelles | 5.3 | 99.1 |
| South Africa | 5.3 | 97.6 |
| Tanzania | 6.8 | 77.9 |
| Tunisia | 7.0 | 95.6 |
| Uganda | 3.6 | 80.8 |
| Zambia | 1.8 | 71.8 |

*Chanzo: Benki ya Dunia, Indiketa za Maendeleo ya Kidunia (Shirika la Fedha Duniani-IMF), 2012*

NIMES
keeping development on track

**WIZARA YA UGATUZI NA MIPANGO**
SLP 30005 (00100) Nairobi, Kenya
Simu: +254-020-2252299
www.devolutionandplanning.go.ke

KENYA VISION 2030

WORLD BANK

giz

EMBASSY OF SWEDEN